# Nipashe

Jumanne Septemba 29, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580353

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Jela miaka 20 kwa kubambwa hifadhini na miguu ya nyumbu

UKURASA 4




UKURASA 11

# Polisi watawanya wafuasi CHADEMA



• **Walikuwa** wakimsubiri Lussu, pia watoa sababu, mwenyewe aweka msimamo... *Endelea ukurasa 2*



Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, akihutubia wananchi katika mkutano wa kampeni kwenye uwanja wa CCM Samora, mjini Iringa jana. **PICHA: IKULU**

# Kishindo cha JPM awamu ya tatu kampeni

UK. 2



Mgombea wa urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha ADA-TADEA, Juma Ali Khatib (kushoto), akipeperusha bendera ya chama hicho, kuashiria uzinduzi wa kampeni za uchaguzi mkuu katika kiwanja cha Magaeni Sogea, Zanzibar jana. Kulia ni mgombea mwenza wake, Hassan Kijogoo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wagombea urais vyama 6 walia ukata

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play | Download on the App Store

Fursa kwa Wagombea! 2020

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

# Wafuasi CHADEMA watawanywa kwa mabomu

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi Mkoa wa Kipolisi wa Tarime/Rorya, limetumia mabomu ya machozi kuwatawanya wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), waliokuwa wamejikusanya katika eneo la Nyamongo, mkoani Mara.

Wafuasi hao walikuwa wamekusanyika kusubiri msafara wa mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano kupitia chama hicho, Tundu Lissu, aliyekuwa akitokea Tarime Mjini kuelekea Serengeti.

Baada ya Polisi kupiga mabomu ya machozi, kulitokea mabishano ya muda mfupi kati yao na Lissu ambaye alionyesha kutokuridhishwa na hatua hiyo ya kuwadhibiti wafuasi wake.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tarime/Rorya, William Mkonda, alisema walilazimika kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya wafuasi wa chama hicho ambao walikuwa wakishambulia askari polisi.

Mgombea huyo aliwaambia polisi kuwa kama eneo hilo halikuwa la mkutano basi walipaswa kupeleka malalamiko yao kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), badala ya kuwazuia kwa kupiga mabomu ya machozi.

"Sheria inasema kama una malalamiko, unakwenda kwenye Kamati ya Maadili ya NEC na siyo kuwapiga watu mabomu, sasa wewe amua nilale hapa, wewe unipige mabomu au unipige risasi, lakini hapa siondoki," alisikika Lissu akijibizana na polisi waliokuwa katika eneo hilo la Nyamongo.

Kamanda Mkonda, alisema wafuasi hao wa CHADEMA walikuwa wakishambulia askari kwa kutumia mawe baada ya kukatazwa kufanya mkutano eneo ambalo halikuwa kwenye ratiba yao.

"Msafara wa Tundu Lissu, haujashambuliwa, isipokuwa askari walikuwa wakiwadhibiti wafuasi wa CHADEMA ambao walikuwa wakiwashambulia Polisi baada ya kukatazwa kufanya mkutano katika eneo ambalo halikuwa kwenye ratiba ya chama hicho," alisema Mkonda.

"Tumepiga mabomu ya machozi kwa watu waliokuwa wanawarushia mawe askari wa Jeshi la Polisi na hadi sasa msafara wa Tundu Lissu uko njiani kuelekea Serengeti na unaongozwa na Polisi," alisema Mkonda.

Mkonda alisema Jeshi la Polisi lilijitahidi kuimarisha usalama wa mgombea huyo wa urais tangu alipofika Tarime na mpaka alipoondoka jana.

Wakati huo huo, Lissu alisema kwamba hajapata wito rasmi kutoka (NEC), unaomtaka kwenda kwenye Kamati ya Maadili na hatarajii kuacha kampeni kwenda kuitika wito wa mitandaoni.

Lissu ameandika hayo kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa 'twitter'.

Juzi, NEC kupitia Mkurugenzi wake, Dk. Charles Mahera alisema wamemwandikia barua mgombea huyo wa urais kupitia CHADEMA, kumuita mbele ya Kamati ya Maadili leo Septemba 29.

Kwa mujibu wa NEC inamtaka Lissu ajibu tuhuma alizozitoa hivi karibuni akidai Rais Dk. John Magufuli alikutana na wasimamizi wa uchaguzi ngazi ya majimbo ili kuhujumu Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Dk. Mahera alisema kuwa, Lissu akiwa Musoma mkoani Mara Septemba 26 mwaka huu, alisikika akisema kuwa mgombea wa CCM, Dk. John Magufuli aliitisha kikao na kukutana na wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo yote nchini jijini Dodoma kwa ajili ya kupanga mipango ya kuhujumu uchaguzi.

Kupitia ukurasa wake huo, Lissu aliandika kwamba; "Sijapokea malalamiko yoyote juu ya jambo lolote linalohusiana na kampeni za uchaguzi mkuu huu kutoka NEC. Sitarajii kuacha kampeni ili kuitikia wito wa mitandaoni wa mtu yeyote," alisema katika tweet yake.



Mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, akizungumza na wananchi katika mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu kwenye viwanja vya Mnyabuhimilwa, mkoani Geita juzi. **PICHA: BONIFACE GIDEON.**

## Mgombea urais SAU sasa kuja kisayansi

**Na Sabato Kasika**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha Sauti ya Umma (SAU), Muttamwega Mgaywa, amesema siku yoyote kuanzia sasa ataibuka kufanya awamu ya pili ya kampeni zake alizodai kwamba, zitakuwa za kisayansi.

Alisema hayo jijini Dar es Salaam jana alipokuwa akizungumza na gazeti hili kuhusu kimya chake cha wiki moja bila kufanya kampeni na kufafanua kuwa alikuwa anajipanga upya.

"Tulizindua kampeni pamoja na ilani Septemba 13, mwaka huu, tukaendelea kwa siku kadhaa kisha tukaamua kujipanga upya, kwa sababu tunataka kampeni za kisayansi," alisema Mgaywa.

Bila kufafanua zaidi kuhusu mbinu hizo za kisayansi, mgombea huyo alisema, kinachofuata sasa ni yeye kwenda mikoani kujinadi kwa siku zilizosalia kabla kufanyika kwa uchaguzi mkuu Oktoba 28 mwaka huu.

"Ratiba kamili itajulikana siku chache zijazo, lakini jambo la muhimu ni kwamba wanachama wetu na Watanzania kwa ujumla wajue kuwa sasa tunajiandaa kuwafuata huko waliko," alisema.

Mgaywa alisema, chama chao kimejipanga kufanya kampeni za kistaarabu kwa lengo la kuibuka na ushindi na kwamba ndiyo maana kimekaa kimya kwa muda kikipanga mikakati ya ushindi.

Alisema, anajua wagombea wengine wa urais wanaendelea na kampeni, lakini aliongeza kuwa kutangulia si kufika, na kwamba kinachotakiwa ni kuwa na mikakati ya kuibuka kidedea.

Alisema, SAU nayo itazunguka nchi kuomba kura kwa Watanzania, wakiwamo wanyonge ambao amedai kwamba, chama chao kinataka kuwatetea hasa wakulima, ambao ndiyo wengi nchini.

# JPM aanza kampeni awamu ya tatu urais kwa kishindo

**Na Gwamaka Alipipi, IRINGA**

MGOMBEA urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, jana alianza awamu ya tatu ya kampeni zake kwa kishindo huku akiahidi neema kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara.

Akihutubia maelfu ya wanachama na wapenzi wa CCM waliofurika katika Uwanja wa Samora mjini hapa, Magufuli alisema iwapo atachaguliwa kwa mara nyingine kuwa Rais, makundi hayo yatapewa kipaumbele katika kuchagua maendeleo ya nchi.

Alisema Ilani ya Uchaguzi ya CCM yenye ukurasa 303, imeyagusa kwa asilimia kubwa makundi hayo kwa miaka ijayo kwa kuwatengenezea mazingira bora ya utendaji, ufanyaji biashara na kuwainua kutoka katika umaskini.

Rais Magufuli alisema lengo lake kubwa ni kuibadilisha Tanzania kuwa nchi ya kujitegemea, pamoja na kuwatoa Watanzania katika umaskini.

**WAKULIMA**

Kuhusu wafugaji, Rais Magufuli alisema CCM itahakikisha inaongeza maeneo ya umwagiliaji kwa hekta 111,192, kwa kukamilisha ujenzi wa skimu za umwagiliaji 261 katika mikoa 25, kati ya hizo skimu ndogo ni 179, za kati 63 na kubwa 19.

Pia alisema kutajengwa na kuimarisha mabwawa 88 ya uvunaji wa maji ya mvua 88 katika skimu za umwagiliaji kwa ajili ya kilimo cha mpunga na mazao mengine katika mikoa 25.

"Tutahakikisha tunashughulikia upatikanaji wa mbolea, viuatilifu, dawa, kuanzisha mifumo ya bima kwa wakulima, kuhamasisha watu kuanzisha viwanda vidogo vya kuhudumia kilimo na upatikanaji wa mitaji kwa wakulima wadogo," alisema Dk. Magufuli.

Sambamba na hilo, alisema kutakuwapo na mkakati wa kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika kilimo cha kisasa cha kibiashara hususani ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na kuwashirikisha wakulima kila mwaka.

**WAVUVI**

Dk. Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano ijayo, serikali ya CCM itahakikisha sekta ya uvuvi inaimarika kwa kuongeza matumizi ya sayansi na teknolojia ya uvuvi endelevu ili kuhimili ushindani na kufanya nchi kujitosheleza kwa mahitaji ya samaki na kuachana na uagizaji kutoka nje.

Pia alisema serikali ijayo itawezesha mauzo ya bidhaa za wavuvi nje ya nchi ili kuchangia zaidi katika ukuaji wa uchumi wa taifa, kuzalisha ajira nyingi kwa vijana na kuboresha maisha yao.

**WAFANYABIASHARA**

Kuhusu wafanyabiashara, alisema katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itahakikisha mchango wa sekta ya biashara kwenye pato la taifa unaendelea kuimarika na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi na wananchi.

Alisema serikali itahakikisha kunakuwapo na mazingira wezeshi ya biashara sambamba na upatikanaji wa fursa nafuu za kibiashara ili kuchochea ujenzi wa viwanda na uzalishaji wa bidhaa zenye ubora wa kimataifa na zinazohimili ushindani.

Kwa mujibu wa Magufuli, pia kutafanyika kwa mapitio na maboresho ya sera na mikakati mbalimbali itakayoimarisha mazingira ya ufanyaji biashara pamoja na kukuza biashara ndani na nje ya nchi.

**WAFUGAJI**

Kadhalika, Dk. Magufuli alisema miaka mitano CCM itaendelea kuleta mabadiliko makubwa na ya kisayansi katika ufugaji kwa kuhimiza ufugaji wa kisasa ili kuzalisha ajira nyingi hususani kwa vijana.

# Mgombea urais aahidi kufuata nyayo za Shein

**Na Rahma Suleiman,** Zanzibar

MGOMBEA urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha ADA- TADEA, Juma Ali Khatib, amesema akichaguliwa kuwa rais wa Zanzibar anakusudia kufuata nyayo za rais Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuendeleza na kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati, ambayo lengo lake kubwa ni kukuza uchumi na kuongeza ajira kwa vijana.

Khatib alisema hayo wakati akizindua kampeni za chama chake katika uwanja wa Magaeni Sogea, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema miradi yote muhimu iliyobaki, ambayo imesimamiwa na Rais Shein anakusudia kuimaliza, ili kuunga mkono kazi nzuri iliyofanywa katika kipindi cha miaka kumi ya uongozi wake.

"Nikichaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar, nakusudia kutekeleza miradi yote muhimu ya kimkakati ikiwamo ujenzi wa bandari ya Mpigaduri iliyopo Maruhubi, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja...nitajenga uwanja wa ndege wa Karume uliopo Pemba, ili kuruhusu kutua ndege kubwa na kuongeza idadi ya watalii," alisema.

Khatib ambaye ni waziri asiye na wizara maalumu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, alimshukuru Rais Dk. Shein kwa kumjumuisha katika Baraza la Mawaziri na hivyo kupata uzoefu wa hali ya juu wa uongozi.

"Namshukuru Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kuniteua kuingia katika Baraza la Mawaziri na hivyo kupata uzoefu mkubwa wa uongozi," alisema.

Alisema akichaguliwa kuwa rais, anakusudia kufufua eneo la viwanda vidogo liliopo Amani kwa ajili ya kuzalisha ajira nyingi za vijana na kurudisha enzi ya Zanzibar ya kupiga hatua kubwa katika sekta hiyo.

Pia, alisema katika miaka ya 1980, Zanzibar ilikuwa maarufu kwa kuwa na viwanda vingi vidogo vya aina mbalimbali ikiwamo masufuria, sabuni, nyaya za umeme pamoja na mafuta ya nazi na kusafirisha nje ya nchi.

"Mimi nilibahatika kufanya kazi katika Shirika la viwanda vidogo viliopo Amani...tulikuwa tukizalisha bidhaa mbalimbali na kusafirisha nje ya nchi," alisema.

# Wagombea urais vyama 6 wakabiliwa ukata

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAGOMBEA urais wa vyama sita, wamezungumzia siku 30 za kampeni waliyoifanya huku wengine wakisema kuifikia mikoa yote, kwa siku zilizobaki itakuwa ngumu kutokana na ukata unaovikabili vyama vyao.

Wagombea hao pia wamelaani kauli za uchochezi zinazohatarisha kuvunjika kwa amani nchini, zinazotolewa na baadhi ya wagombea wa nafasi hiyo.

Kampeni za wagombea kwa vyama vyote zilianza rasmi Agosti 16 na zitahitimishwa Oktoba 27, mwaka huu na kutoa fursa kwa wananchi kushiriki kupiga kura Oktoba 28.

**UPDP**

Wakizungumza katika mahojiano jana kwa nyakati tofauti, mgombea urais kupitia Chama cha UPDP, Twalib Ibrahimu Kadege, alisema hadi sasa ameifikia mikoa minne pekee kwenye kampeni kati ya zaidi ya mikoa 27, ya Tanzania Bara na Zanzibar.

"Uwezekano wa kuifikia mikoa yote itategemeana na uwezeshaji, chama chetu hakina ruzuku kwa hiyo wanachama ndio wanachangishana ndipo mgombea urais, aweze kusafiri kwenda kwenye kampeni," alisema.

**NRA**

Naye mgombea urais kupitia Chama cha NRA, Leopold Mahona, alisema tangu aanze kampeni amefanikiwa kuifikia mikoa 13 na kwamba na anatarajia kuifikia mikoa yote.

Mahona alisema katika siku zilizobaki za kampeni, anatarajia kuanza kutumia helikopta kwa kufanya mikutano 20, kila siku.

Kuhusu uchochezi, alisema wagombea wenzao wenye vyama vyenye wafuasi wengi, ndio watakaokuwa chanzo cha kuvunjika kwa amani nchini kutokana na kauli zao zisizo na mashiko.

"Tuache masuala ya kuchezea amani ya nchi, kila mgombea aombe kura kwa wananchi kwa kutumia hoja na ushawishi na vipaumbele vyake," alisema Mahona.

**DEMOKRASIA MAKINI**

Mgombea urais kupitia Chama cha Demokrasia Makini, Cecilia Mwanga, alisema hadi jana amefanikiwa kuifikia mikoa miwili pekee, katika kampeni na kwamba amepanga kufika mikoa minane pekee.

Mmanga aliwatahadharisha wagombea wenzake kuacha kutoa lugha zinazohatarisha kuvunjika kwa amani kwa kuwa ikivunjika watakaoathirika ni pamoja na familia na ndugu zao.

**ADC**

Mgombea wa Chama cha ADC, Queen Sendiga, alisema amefanikiwa kuifikia mikoa minane tangu kampeni zimeanza, mitano ya Zanzibar na mitatu ya Tanzania Bara.

Alisema atahakikisha muda uliobaki anaifikia mikoa yote na maeneo mengine anatumia mfumo wa kuwafuata wananchi katika maeneo yao, badala ya kuitisha mkutano wa hadhara wa kampeni.

**DP**

Mgombea wa urais kupitia Chama cha DP, Philipo Fumbo, alisema ameifikia mikoa minane hadi sasa na malengo yake ni kufikia mikoa yote.

Fumbo alilaani kauli za kichochezi zinazotolewa na baadhi ya wagombea wenzao na kuwataka kufanya kampeni za kistaarabu, ambazo zitalinda amani iliyopo nchini.

**AAFP**

Naye mgombea urais kupitia Chama cha AAFP, Seif Maalim Seif, alisema ametembelea mikoa 15 katika kampeni na amepanga kuifikia yote.

Seif alisema kuna umuhimu wa kufanya mabadiliko ya namna ya kuendesha kampeni kwa kuachana kutumia mikutano ya hadhara ya kampeni, ambayo ndio inakuwa kichocheo kwa baadhi ya wagombea kutoa kauli zinazohatarisha amani ya nchi.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, akifungua mkutano wa viongozi wa dini na siasa wa kuhamasisha amani na haki nchini, ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), jijini humo jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Viongozi wa dini wawapigia debe wanawake kuchaguliwa

**Na Bearrice Moses,** TUDARCo

KAMATI ya Amani ya Viongozi wa Dini imebainisha kuwa inaamini wanawake wakichaguliwa kwenye nafasi za uongozi watakuwa na fursa ya kutunga sera na kushiriki katika vyombo vya maamuzi, hivyo watakuwa chachu ya kuleta maendeleo na mapinduzi ya kiuchumi nchini.

Imebainisha kuwa zipo sababu nyingi zinazomkwamisha mwanamke katika nafasi ya uongozi na moja ya vikwazo kwake kupata uongozi ni uwapo wa mfumo dume ndani ya vyama vya siasa.

Hayo yamebainishwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Sheikh Alhad Salum, wakati akizungumza kwenye warsha ya siku moja kuhusu nafasi ya mwanamke kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba katika mustakabali wa haki, heshima, amani na utulivu kuchagua viongozi bora.

"Ikumbukwe wanawake ni zaidi ya nusu ya idadi ya watu duniani, hivyo ili kutokomeza umaskini, lazima wanawake wapewe nafasi kikamilifu, Biblia inasema "wanawake watangazao habari ni jeshi kubwa(zaburi 68:11b) hivyo ni wazi wanayo nguvu ya kufanikisha hili," alisema.

Alisema vyama vingi vya siasa vinawatumia wanawake katika shughuli za uhamasishaji, kuongeza idadi ya wanachama na kueneza sera za vyama hivyo, ikiwamo wakati wa kampeni katika kuwavutia wapigakura, lakini kwa asilimia kubwa hawawatumii kama wadau kwa kuruhusu wapewe nafasi za uongozi zenye nguvu ya maamuzi.

Kamati hiyo pia imetumia fursa hiyo kuvitaka vyama vya siasa kutanguliza uzalendo mbele kwa maslahi mapana ya nchi.

"Sote kwa pamoja tukemee na kuwaelimisha wafuasi wetu kuondokana na vitendo vyote vyenye kuashiria uvunjifu wa amani, ugomvi, matusi, kejeli hayo yote siyo utamaduni wetu, tuendeleze utamaduni wa kuhojiana kwa hoja," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Rose Reuben, alisema wameandaa warsha hiyo ili kumewakutanisha viongozi wa dini na wa kisiasa wa Mkoa wa DSM na baadhi ya wadau wengine ili kuwapa nafasi kujadili kwa pamoja kuhusu nafasi ya mwanamke kuelekea Uchaguzi Mkuu Oktoba 28, 2020.

Alisema kwa sasa kuna asilimia 37 tu ya viongozi wanawake waliopo kwenye ngazi za maamuzi bungeni, na kwamba bado kuna mapengo katika ushiriki wao ambapo yanapaswa kuzibwa.

"Kuna mapengo pamoja na nguvu ndogo ya mwanamke kiuchumi, rushwa ya ngono inayotajwa kutumika wakati wa uchaguzi, rushwa ya kifedha, uchumi duni kwa wanawake wanaotaka kugombea, hivyo kusababisha kushindwa kufanya kampeni,"

Awali Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salam, Abubakar Kunenge, aliyekuwa mgeni rasmi kwenye warsha hiyo alisema viongozi wa dini wanategemewa katika kuhamasisha amani na mshikamano nyakati zote ikiwamo wakati huu wa kampeni na uchaguzi mkuu, hivyo anaamini viongozi hao watatumia vyema nafasi zao na siyo vinginevyo.

# Miaka 20 jela kwa kukutwa hifadhini na miguu ya nyumbu

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKAZI wa Kijiji cha Karagatonga, Tarafa ya Ingwe wilayani Tarime, mkoani Mara, Chacha Magoko, amehukumiwa kwenda jela miaka 20, kwa kupatikana na hatia ya makosa ya kuingia Hifadhi ya Taifa Serengeti bila kibali, kukutwa na silaha na nyara za serikali.

Kabla ya kusomewa hukumu ya uhujumu uchumi na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya Tarime, Visensia Balyaruha, awali wakili wa serikali kitengo cha TANAPA, Bulembo Kasika, alidai kuwa mshtakiwa Magoko, Februari 14, mwaka huu, alikamatwa na askari wa wanyamapori akiwa ameingia ndani ya Hifadhi ya Serengeti bila kibali, akiwa na nyaya za kutegea wanyama, mkuki, kisu, nyara za serikali miguu miwili ya nyumbu yenye thamani ya Sh. 1,848,000.

Mshtakiwa alikana mashtaka hayo na upande wa mashtaka ulileta mashahidi wanne na vielelezo alivyokutwa navyo mshtakiwa huyo vikiwamo nyara na silaha hizo.

Upande wa mshtakiwa haukuwa na shahidi yeyote mbali na maelezo yake aliyotoa mbele ya mahakama hiyo, huku akiomba kupewa adhabu ndogo kwa kuwa ni tegemeo la wadogo zake na hana wazazi.

Wakili wa TANAPA, Kasika aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa, ili iwe fundisho kwa watu wengine wanaoangia ndani ya hifadhi za taifa na kuhujumu kwa kuwaua wanyama, ambao ni rasilimali ya taifa inayoingizia serikali mapato kwa ajili ya maendeleo.

Hakimu Visensia alimhukumu mshtakiwa kwa kupatikana na makosa yote matatu la kwanza la kuingia hifadhini bila kibali alimhukumu kulipa faini Sh. 300,000 ama kifungo cha mwaka mmoja jela, kosa la pili kupatikana na silaha za jadi ndani ya hifadhi, kwenda jela mwaka mmoja au faini ya Sh. 300,000 na kosa la tatu la kupatikana na nyara za serikali miguu miwili ya nyumbu, kwenda jela miaka 20.



Wafanyakazi wa kampuni ya CCECC inayojenga barabara za juu za mpishano Ubungo, jijini Dar es Salaam, wakifanya ukarabati wa mwisho jana, kwa ajili ya kuruhusu magari kupita juu kutoka Barabara ya Sam Nujoma hadi ya Mandela. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**



## Heche amkabidhi Lissu kero

**Na Timothy Itembe,** MARA

MGOMBEA ubunge Jimbo la Tarime Vijijini kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Heche, amemkabidhi kero za mji wa Sirari mgombea urais kupitia chama hicho, Tundu Lissu, ili kuzishughulikia endapo atachaguliwa na wapiga kura.

Heche alisema kuwa, wakazi wa mji wa Sirari wanakabiliwa na changamoto ya kubambikiwa kesi za kuwa sio raia wa Tanzania wanapojitokeza kugombea hususani kupitia tiketi ya CHADEMA.

"Nikuombe mgombea wetu wa nafasi ya rais endapo wapigakura watakuamini na kukuchagua, uhakikishe kuwa unamaliza kero iliyopo ya watu wa Sirari ya kubambikiwa kesi kuwa wao sio Watanzania hususani wale wanaokuwa wanajitokeza kugombea nafasi za uongozi kupitia CHADEMA," alidai.

Heche aliongeza kuwa mahitaji makubwa ya wakazi wa mpakani wanategemea bidhaa kutoka nchi jirani ya Kenya kwa sababu gharama ni nafuu ya kununulia ikilinganishwa na bidhaa za Tanzania.

# Watanzania kufikia mil. 185 mwaka 2065

**Na Christina Mwakangale,** TANGA

ONGEZEKO la idadi ya watu nchini, linatajwa kuwa mara mbili kila baada ya miaka 23, huku ikikadiriwa mwaka 2065 kutakuwa na Watanzania milioni 185.

Hayo yalibaishwa jana jijini hapa na Mkurugenzi Mtendaji wa Ujuzi.Era, Dastan Kamanzi, ambaye ni mwandaji wa kitabu cha mwongozo kwa waandishi wa habari kuhusu mchango wa vyombo vya habari kuhakikisha gawio sawa kulingana na idadi ya watu.

Mwongozo huo ambao umetolewa na Baraza la Habari Tanzania (MCT), umekwenda sambamba na maadhimisho ya siku ya kimataifa ya upatikanaji wa taarifa, ijulikanayo Kama 'Siku ya Haki ua Kujua'.

Akifafanua kuhusu mwongozo huo, Kamanzi alisema utafiti uliofanywa na MCT ulibaini, asilimia 94 ya Watanzania ni tegemezi ni makundi mawili, ambayo ni watoto kati ya umri 0 hadi miaka 14 na wazee wenye miaka 65 na kuendelea.

Alisema kutokana na ongezeko hilo, nchi iwekeze katika elimu, afya, uchumi rasilimali watu na utawala ili kuwapunguzia mzigo wanaotegemewa na kundi hilo, ambao ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 64.

"Kila mwanamke wa kitanzania inakadiriwa kuzaa watoto saba, ikifika watu milioni 185 itakuwaje? Na wazalishaji ni asilimia sita tu ambao ni vijana, wadau wanahitaji kuwekeza kiuchumi 'media' zina mchango mkubwa," alisema Kamanzi.

Alisema kunahitajika kuzingatiwa sera, mipango, mikakati, sheria huku waandishi wa habari wakitakiwa kujenga hoja, kufuata maadili pamoja na kuuliza maswali yenye mantiki kitaaluma.

"Haya yaliyoandikwa katika mwongozo huu, mwandishi atakuwa amechangia nchi ipate gawio sawa kulingana na idadi ya watu, ufanyike utafiti, zifuate taratibu kwenye kuandaa habari," alisema Kamanzi.

Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mkajanga, awali akizungumza kuhusu siku ya kimataifa ya upatikanaji taarifa, alisema baraza limebaini kuuna changamoto ya upatikanaji taarifa kutoka kwa vyanzo husika.

Alibainisha kwamba, utafiti kwenye mikoa 18 nchini, uliofanyika Septemba mwaka jana, ulibaini watafuta taarifa baadhi yao walioshiriki utafiti huo, walitishiwa na kukamatwa katika mchakato wa kuzipata.

"Ipo haja ya kuongeza uelewa miongoni mwa watoa taarifa kuhusu Sheria ya Kupata Taarifa ya Mwaka 2016, ili ieleweke na kurahisisha upatikanaji taarifa," alisema Mukajanga na kuongeza...

Serikali iwapatie mafunzo maofisa habari wa serikali ili kuinua wao kuhusu umuhimu wa upatikanaji taarifa, na kuhudumia wananchi."

MAKALA

# Likizo ya corona ilivyokuwa hatari kwa wanafunzi

**Na Zuwena Shame**




MWISHONI mwa mwaka jana, dunia ilikumbwa na baa la mlipuko wa virusi vya corona vilivyoripotiwa kwa mara ya kwanza Wuhan, China na baadaye kusambaa katika mataifa mbalimbali.

Takwimu hadi kufikia Agosti 13, mwaka huu saa 3:35 asubuhi zinaonesha kuwa kuna wagonjwa 20,827,637, vifo 747, 584 katika nchi zote zilizokubwa na corona.

Nchini Tanzania, mgonjwa wa kwanza wa corona aliripotiwa Machi 16 mwaka huu na siku moja baadaye, Serikali kupitia kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ilitangaza kuzifunga shule na vyuo vyote.

Serikali ilichukua hatua hizo ili kupunguza kasi ya kuenea kwa maambukizo ya corona nchini hatua iliyowalazimu wanafunzi kurudi nyumbani kwa likizo ya lazima.

Katika kipindi cha likizo ya ugonjwa wa corona tatizo la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi ilijitokeza halikuachwa nyuma katika maeneo mengi nchini ikiwamo Manispaa ya Kinondoni Mkoa wa Dar es Salaam.

Ukatili wa kijinsia umeripotiwa pia katika vituo mbalimbali vya polisi kwenye dawati la jinsia, hospitalini hasa kwa Maafisa Ustawi wa Jamii, kwa walimu na katika taasisi zisizo za kiserikali. Katika kipindi hicho, baadhi ya watoto walitelekezwa, hawakuangaliwa wala kuhudumiwa ipasavyo na wazazi wao kwa sababu za changamoto zilizowapata wazazi kutokana na maambukizi haya mfano msongo, kuugua, hofu hata kupoteza vyanzo vya mapato. Kutokana na haya, watoto walikosa uangalizi, kupata chakula cha kutosha, kupigwa, kuchomwa moto, kubakwa na hata kukosa mapenzi kutoka kwa wazazi.

Mkurugenzi wa taasisi ya Wanawake katika Jitihada za Maendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza anasema wakati wa likizo ya corona matukio ya unyanyasaji wa kijinsia yalijitokeza nchini ambapo matukio kadhaa yaliripotiwa na taasisi yake.

Anasema kulikuwa na watoto zaidi ya saba walioripotiwa kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kingono na wengine wawili walisurika kubakwa.

Mawinza anasema matukio mengine ni ukatili wa kimwili ambapo watoto wanne walipigwa huku mwingine akichomwa moto na baba yake mzazi.

Anaongeza kuwa katika kipindi hicho matukio hayo yalionekana kuongezeka kwa kasi kubwa kwasababu watoto walikuwa nyumbani wakati wazazi wao wakiendelea na shughuli nyingine.

"Watoto kipindi chote cha likizo ya corona walikuwa wanajichunga wenyewe walikosa uangalizi wa pamoja kama vile wanapokuwa shule hivyo kuzagaa mitaani na kuwa katika mazingira hatarishi zaidi ambapo baadhi yao walifanyiwa vitendo vya ukatili," anasema Mawinza.

Hata hivyo Mawinza alisema kumekuwa na mabadiliko baada ya wanafunzi kufungua shule kwani kesi za ukatili wa kijinsia zimeanza kupungua kwani watoto wengi wapo shuleni ambapo kuna uangalizi.

Mawinza alisema kuwa kesi zaidi ya tano ziliweza kuripotiwa polisi lakini hakuna hata kesi moja au mtuhumiwa aliyepelekwa mahakamani kwa ajili ya kuchukuliwa hatua zaidi mfano kufungwa au kutozwa faini.

Aliongeza kuwa jamii bado inaona kama vitendo hivi ni vya kawaida kufanyiwa watoto kitu ambacho sio sawa hivyo juhudi za makusudi kabisa zinahitajika ili kuweza kuwagundua wanaotenda vitendo hivyo na kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Hii ni kutokana na jamii kukosa uelewa kuhusu haya maswala au pia jamii inafumbia macho maswala haya ya ukatili wa kijinsia. Nawaasa jamii kwa ujumla kuweza kuwa macho na kutokaa kimya, pindi vitendo kama hivyo vinapotokea basi viweze kuripotiwa mara moja ili kuwalinda watoto wetu" alisema Mawinza.

Mawinza alisema kuwa bado elimu zaidi inahitajika kwa jamii kuhusu unyanyasaji wa kijinsia, viashiria vya ukatili, mbinu wanazotumia watenda ukatili na namna ya kuchukua hatua dhidi ya watenda vitendo hivyo.

Alisema kuwa ili kuondoka na vitendo hivi jamii kuanzia ngazi ya kaya kuwa macho kwa kumlinda mtoto wake na wenzake kwani vitendo hivi vimeshamiri kwa kasi katika jamii nyingi nchini.

Kwa upande wake Ofisa Ustawi wa Jamii Mwandamizi, Halili Katani kutoka Hospitali ya Mkoa ya Mwananyamala, alikiri kuwapo kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia katika likizo ya corona na kutolea mfano kesi ya baba mzazi kumfanyia ukatili wa kingono.

Katani alisema kuwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kama vitendo vya kingono kwa watoto mara nyingi hutendwa na watu wakaribu na wanaoaminiwa na familia au jamii hivyo kuwa vigumu kugundua mapema au katika hatua za awali.

Alitolea mfano wa baba mzazi, baba wa kambo, mjomba, kaka na mara nyingine kuwarubuni kwa zawadi kama pipi, chipsi, soda ambapo wengi huwapa watoto hao vitisho kama kuwaua ili wasiseme kwa watu.

Alisema kuwa baba mzazi wa mtoto (jina linahifadhiwa) alifanya kitendo hicho kipindi cha ugonjwa wa corona ambapo mtoto alikua nyumbani. Alianza kujenga tabia ya kumuogesha na kuwa naye karibu muda mwingi huku akiwa na lengo tofauti kabisa na malezi au mapenzi na mtoto wake.

Aliongeza kuwa ilikuwa vigumu kwa mama mzazi na majirani kugundua mapema kitendo hicho kwani mtoto naye aliona ni jambo la kawaida kwake na halina madhara yoyote kwakuwa alikuwa anafanyiwa na baba yake mzazi, mtu anayemuamini.

Aliongezea kuwa vitendo hivyo mara nyingi hufanyiwa watoto wadogo na wale wa shule za msingi kwani wengi wao hawana elimu jinsi ya kugundua pindi wanapofanyiwa vitendo hivyo na wapi kwa kuripoti au kutoa taarifa pindi wanapoona wanafanyiwa ukatili huo.

Alisema kuwa katika kipindi cha likizo ya corona kesi kama za mimba ziliweza kujitokeza lakini wasichana wengi walitoa kisingizio cha maisha magumu na umaskini hivyo kufanya vitendo hivyo kama njia mojawapo ya kuweza kujikimu kimaisha katika familia zao.

Alisema kuwa wanafunzi wengi waliopata ujauzito ni wale wa sekondari na kuongezea walidai hali ngumu na kiuchumi za wazazi wao zinachangia wao kijiingiza kwenye maswala ya kingono.

"Wanafunzi hawa wanajua athari za vitendo vya ukatili kwakuwa tunawapa elimu kwa kupita katika mashule . Wanajua wapi kwa kuripoti na jinsi ya kujikinga ila wengi wao walisema kuwa wazazi wao hawako vizuri kimaisha hivyo kuwalazimu wao kujiingiza kwenye vitendo vya ngono na kuweza kujipatia kipato cha kujikimu kimaisha" alisema Halili.

Alisema kuwa sio sawa kwa wanafunzi kukaribisha vitendo vya ukatili mfano ngono kwa kisingizio cha maisha magumu kwani kina madhara ya maradhi mbalimbali kama magonjwa ya zinaa mfano ugonjwa wa UKIMWI kwani wanaweza kukatisha ndoto zao za baadae za kimaisha na kiuchumi pia. Alisema kuwa vitendo hivi vinahitaji kupigwa vita na hivyo kuwepo ushirikiano baina ya jamii nzima, serikali na wadau mbalimbali kama shirika la Save the Children ambalo limekuwa mstari wa mbele katika kusaidia kutoa elimu kwa watoto Pamoja na walezi.

Alisema kuwa Save the Children imekuwa inafanya kazi kwa ukaribu Zaidi na Serikali na wadau wengine katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia na haki za watoto.

Alisema kuwa kwa upande wa Serikali imeweka maofisa ustawi wa jamii katika vituo vya afya, zahanati na shule au namba za simu za bure kwa kutoa taarifa sehemu husika pindi vitendo vya ukatili vinapotokea katika jamii. Kwa kipindi ambacho watoto wapo shuleni hawanabudi kuendelea kulindwa na kuelimishwa juu ya kujilinda dhidi ya maambukizi ya ugonjwa huu wa virusi vya Corona.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Wazazi na walezi tuacheni mila zinazokwamisha elimu*

**ILI** mabinti wa Tanzania wapate elimu bora kuna kila sababu ya wazazi na walezi kuachana na tamaduni na mila zinazowaponza hasa kuwaachia watoto kuingia kwenye mafundisho na taratibu ambazo zinawaelekeza kufanya ngono wakiwa kwenye umri mdogo.

Tamaduni hizo ni pamoja kuwacheza mabinti ngoma wanapokaribia kupevuka au kufikia umri wa balehe na haya ni mambo yanayofanyika baada ya wanafunzi kumaliza darasa la saba.

Mwaka huu mtihani huo ambao umesogezwa mbele kutokana na shule kufungwa miezi mitatu ili kuepusha maambukizi ya COVID-19 unatarajiwa kufanyika kuanzia wiki ijayo.

Mabadiliko na kuachana na mila hizo ni jambo la msingi kwa sababu mabinti hao ni wadogo na wengi bado wako shuleni na wanatarajiwa kusoma zaidi hadi sekondari na kufikia vyuo vikuu. Ikumbukwe kuwa serikali inawekeza katika elimu na ndiyo inayogharamia elimu msingi kuanzia msingi hadi sekondari.

Tunashauri kuwa ni vyema jamii ikajielewa na kukubaliana nasisi kwamba kuwacheza watoto wa kike ngoma wakiwa masomoni kunawaathiri kisaikolojia na kusababishwa kushindwa kuendelea na masomo.

Tunaona kuwa ngoma na mafundisho yanayojielekeza kwenye masuala ya ngono ni vikwazo vinavyokwamisha maendeleo ya elimu katika mikoa na jamii zinazoendelea kuenzi mila na desturi zisizo na tija wala ustawi wa taifa.

Tunawahimiza na kuwataka wazazi na walezi kuachana na mila hizo potofu za kuwacheza ngoma watoto wa kike wakiwa bado wanasoma shule kwani wanawaharibu kisaikolojia, kimaadili na hasa katika masomo yao.

Tunaamini kuwa mtoto wa kike anapochezwa ngoma anapohitimu darasa la saba kuanzia mwezi ujao hakumsaidii kwa vile wengi wanakuwa wameandaliwa na kuwekwa tayari kuolewa au kujiingiza kwenye masuala ya ndoa.

Tunawashauri wazazi, walezi na walimu kushirikiana kwani inawezekana wengi hawajafahamu kuwa kufanya hivyo ni kuwandaa kuwa wali wanaosubiri kuolewa?

Aidha, sote tufahamu kuwa ni jukumu letu kusisitiza kuwa ili watoto wa kike wasome kuna kila sababu kama taifa kufanya jitihada za kuwapeleka kwenye njia zilizonyooka badala ya kuwaingiza kwenye mitego.

Lakini pia, tunawashauri viongozi hasa wale wanazungukwa na mila za kuwacheza mabinti ngoma na kuwaingiza kwenye mahusiano wakiwa wadogo, kuona namna ya kupeleka mapendekezo ya kutunga sheria ndogo ndogo zitakazopiga marufuku mabinti wanaosoma kuchezwa ngoma.

Tunayasema haya kwa sababu baadhi ya wazazi na walezi wanasubiri mtihani wa darasa la saba kumalizika ili kuandaa sherehe hizo za ngoma za unyago.

Tunaamini wakati umefika kwa watendaji kata, maofisa elimu kata, kamati za elimu na uongozi wa vijiji kulisimamia hilo na kuwashauri wazazi na walezi kusubiri hadi hapo wasichana watakapomaliza masomo. Tunawakumbusha kuwacheza ngoma watoto ni moja ya sababu inayoshusha ufaulu wa wanafunzi katika mikoa inayoendekeza utamaduni ukiwamo huo wa unyago.

Ni wakati wa kuona kuwa tunawasaidia wasichana kufaulu kwenda shuleni, kuingia darasani na kusoma pamoja kufundishwa ipasavyo.


Lakini sisi wazazi na walezi kusimamia nidhamu ya watoto wetu nyumbani na ndani ya jamii na kuwa karibu nao katika kuwashauri umuhimu wa elimu na kujua namna ya kujitegemea na kuendesha maisha yao sasa.

Tusiiangushe serikali wakati ikitekeleza majukumu yake kwa kuhakikisha kunakuwapo na walimu, miundombinu, vitabu, maabara na kugharamia mahitaji mengine kulingana na kile shule inachohitaji.

Tunawakumbusha wazazi na walezi kuachana na tamaduni ambazo zinakuwa kikwazo kwa watoto kusoma. Tuwalinde watoto wetu wanaomaliza shule wiki ijayo na tuweke utaratibu unaozielekeza shughuli hizo kufanyika baada ya watoto kufikia umri wa kujitambua na kujua mambo mema na mabaya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# *Ilani, vyama safari hii vimeisahau TEHAMA...*

Na Sabato Kasika

**TEKNOLOJIA** ya Habari ya Mawasiliano (TEHAMA), ni chachu ya maendeleo na imeleta mabadiliko makubwa katika nyanja mbalimbali za maisha kuanzia elimu, utamaduni na uchumi.

Kwa kutambua umuhimu wa teknolojia hiyo, mwaka 2005 Tanzania ilianzisha somo la TEHAMA katika mtaala wa elimu ya msingi ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo.

Lengo la kuwapo kwa somo hilo ni kumpa mwanafunzi maarifa na stadi za matumizi ya habari, vyombo vya mawasiliano na maktaba, ambapo hadi sasa baadhi ya shule zinafundisha TEHAMA.

Ufundishaji huo unatokana na shule kuwa na vifaa hasa kompyuta, umeme na wataalamu, ingawa baadhi ya shule hasa za vijijini hazina nishati hiyo.

Kwa ujumla dunia ya sasa utandawazi umesababisha kuenea kasi ya matumizi ya TEHAMA ambayo inapotumiwa kikamilifu inakuwa na fursa kwa wengi kupata elimu, kuleta usawa kielimu, kujenga mazingira na mbinu bora za ufundishaji na kujifunza, kuongeza weledi wa walimu na wataalamu wa teknolojia hiyo.

Vilevile inaimarisha usimamizi wa masuala ya elimu, uongozi na utawala, kwa mazingira ya sasa teknolojia haikwepeki ndiyo maana TEHAMA ni miongoni mwa mambo ambayo serikali inayapa kipaumbele.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, awamu ya tano inatoa kipaumbele kwenye matumizi ya TEHAMA ili kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika utendaji kazi wa shughuli za serikali za kila siku.

Kutokana na hilo, wananchi nao wanahimizwa kutumia teknolojia hiyo ya habari na mawasiliano kwenye shughuli za uzalishaji mali na utoaji huduma katika sekta mbalimbali ili kukuza uchumi na kuongeza ajira.

Hata hivyo, kwenye ilani za uchaguzi za vyama mbalimbali vya siasa, suala ya TEHAMA halikuelezwa na kufafanuliwa kwa uzito kwamba, iwapo vitashinda vitaendelezaje somo hilo nchini.

Vyama vimejikita zaidi katika ahadi za kutoa elimu bure, kuondoa msongamano wa wanafunzi kwa kuongeza vyamba vya madarasa na mahitaji mengine shuleni ambayo kimsingi ni ya muhimu.

Lakini suala la kuboresha somo la TEHAMA ni kama limeguswa kidogo mno ingawa nalo lina changamoto nyingi, ikiwamo ukosefu wa nishati ya umeme kwenye shule nyingi za vijijini hali ambayo si rahisi kuendesha somo hilo.

Ingependeza kama vyama vingezungumzia kwa kina, mikakati ya kuimarisha somo hilo ili kuhakikisha changamoto zinapungua kama siyo kumalizika kabisa ili kuwe na uwiano kati ya wanafunzi wa shule za mijini na vijijini.

Kwa mfano katika ilani ya CHADEMA, ukurasa wa 33, inasema, mitaala ni mikubwa mno na haizingatii mahitaji ya mwanafunzi na mazingira yaliyopo.

Inaongeza elimu imejikita kwenye mfumo wa kikoloni na haiendani na mahitaji ya sasa na malengo ya kiuchumi na kimaendeleo ya jamii ambayo Watanzania wanakusudia.

Inafafanua kuwa mabadiliko ya mitaala hayaendi sambamba na matayarisho ya walimu na maendeleo ya vitabu vya kusomeshea na hakujatolewa mkazo unaostahili wa elimu ya TEHAMA.

Ilani ya CCM, ukurasa wa 152, inaelezea kwamba inakusudia kuimarisha na kuhamasisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika uchumi wa kidijitali, husasan serikali mtandao, miundombinu ya TEHAMA katika nyanja za uchumi na ulinzi wa mitandao.

Jingine ni kutenga fedha kwa ajili kuanzisha vituo vya umahiri vya sayansi na teknolojia, katika taasisi za elimu ya juu nchini kwa kuzingatia maeneo ya kimkakati katika kujenga uchumi imara na endelevu.

CCM pia inakusudia kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyuo vya sayansi na teknolojia na kukarabati karakana na kuziwekea vifaa vya kisasa vya kujifunzia na kufundishia.

Pamoja na hayo, upo umuhimu wa kukiimarisha zaidi TEHAMA katika shule za msingi ili wanafunzi wawe na ujuzi tangu chini, ili wanapofika juu wawe tayari wana uelewa wa kutosha.

## HABARI KITAIFA

# Msajili wa Hazina aagizwa kuchambua bajeti nje ya mfumo

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

OFISI ya Msajili wa Hazina imeagizwa kutochambua bajeti yoyote ya mwaka 2021/22, itakayowasilishwa nje ya Mfumo Mpya wa Uandaaji na Uwasilishaji wa Bajeti na Taarifa za Bajeti kielektroniki (PLANREP) na Maofisa Masuuli wa Taasisi 236 zilizo chini ya ofisi hiyo.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango, Mary Maganga, alipokuwa akifungua mafunzo ya matumizi ya mfumo huo kwa Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma.

Alisema maofisa hao wanatakiwa kuhakikisha kuwa, mpango na bajeti kwa mwaka 2021/22 unaandaliwa na kuwasilishwa kupitia mfumo huo, ambapo uwapo wake utapunguza upotevu wa mapato, kuimarisha na kuchochea uwajibikaji, kuimarisha uchambuzi wa bajeti na ufuatiliaji na hatimaye kuongeza mapato katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Alibainisha kuwa hadi kufika Juni mwaka 2019, serikali ilikuwa imewekeza katika taasisi, mashirika ya umma na kampuni zinazomilikiwa na serikali kwa hisa chache zipatazo 266 zenye uwekezaji wa kiasi cha Sh. trilioni 59.6.

"Uwekezaji huu ni mkubwa na unahitaji usimamizi madhubuti utakaowezesha ongezeko la tija katika ukuzaji wa uchumi na ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi," alisema.

Naibu katibu huyo alisema ili kuwezesha ufanisi katika usimamizi wa mali za umma, ilihitajika mifumo madhubuti ya kielektroniki itakayorahisisha usimamizi wa rasilimali hizo.

Awali, Msajili wa Hazina, Athumani Mbuttuka, alisema ofisi hiyo ikishirikiana na Ofisi ya Rais- TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango ilianzisha mradi wa kusimika mfumo huo ili kuhakikisha serikali inanufaika na uwekezaji inaoufanya na taasisi hizo.

"Mfumo huu wa bajeti, tayari ulishaanza kutumika na Mamlaka za Serikali za Mitaa tangu mwaka 2017/18, na iliamuliwa kuuboresha ili utumike na kila taasisi iliyo chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina. Mfumo huu umejengwa na wataalamu wa ndani kwa kuzingatia matumizi sahihi ya takwimu za kifedha za serikali," alisema.

Mbuttuka alisema jumla ya taasisi 32 zilialikwa katika hatua ya ujenzi wake ili kufanya majaribio ikiwamo zile zinazofanya biashara, kutoa huduma na za udhibiti huku akisema mfumo huo utasaidia kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma katika mashirika na taasisi za umma.

Pia alisema utasaidia upatikanaji wa taarifa za uhakika na kwa wakati na kupunguza gharama katika ununuzi, uundaji, usimikaji, uendeshaji na usimamizi wa mifumo, kupunguza utitiri wa mifumo ya kibajeti ya kielektroniki iliyoanzishwa bila kupata ridhaa ya Wizara ya Fedha na Mipango.




Wachimbaji wadogo wa mgodi wa Nsangano, Nyarugusu mkoani Geita, wakisikiliza maelezo kuhusu mkopo wa vifaa vya uchimbaji kutoka kwa Ofisa Uhusiano wa Benki ya NMB tawi la Geita, Jane Kitalonga, walipotembelea banda la benki hiyo, katika maonyesho ya sekta ya madini, kwenye viwanja vya Bombambili juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maofisa ACT waachiwa, mmoja ashikiliwa

**Na Enock Charles**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimetaja sababu za baadhi ya maofisa wake kukamatwa na Jeshi la Polisi wakiwa katika ofisi za chama hicho Magomeni jijini Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na makosa ya kimtandao na kile kilichoelezwa ni kuzuia jeshi hilo kufanya kazi yake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa chama hicho, Arodia Peter, ambaye ni mmoja wa maofisa aliyekamatwa na kuachiwa kwa dhamana, alisema yeye na ofisa mwingine wa chama hicho aliyemtaja kwa jina la Dahlia Majid, wanatuhumiwa kwa kosa la kuizuia polisi kufanya kazi yao.

Alisema ofisa mwingine aliyemtambulisha kwa jina la Doto Rangimoto akituhumiwa kwa makosa ya kimtandao.

Kwa mujibu wa Arodia, Doto Rangimoto bado anashikiliwa na polisi katika Kituo cha Polisi Osterbay, huku yeye na mwenzake wakitakiwa kurejea tena leo baada ya kuachiwa kwa kudhaminiwa na watu wawili kila mmoja.

"Walitukamata kwa kile walichodai kuwa ni kuzuia polisi kufanya kazi yao, lakini baadaye tuliachiwa kwa dhamana, lakini Doto bado anashikiliwa," alisema Arodia.

Kukamatwa kwa maofisa hao kumekuja ikiwa ni siku chache tu tangu kukamatwa kwa msaidizi wa Mshauri Mkuu na mgombea urais wa chama hicho, Bernard Membe, kwa tuhuma za utakatishaji fedha jambo lililozua sintofahamu kwa wafuasi wa chama hicho.

# Serikali yaboresha mitaala kujifunzia

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imeboresha mitaala ya kujifunzia kwenye vyuo vya mafunzo ya kilimo nchini ili kuzalisha wataalamu wenye ujuzi stahiki watakaoajiriwa na kujiajiri.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, aliyasema hayo jana kwenye kikao cha pamoja na wajumbe wa Sekta Binafsi, Baraza la Ujuzi wa Kilimo Nchini (TPSF-ASSC), walipokutana jijini hapa.

Alisema lengo la serikali ni kuzalisha maofisa ugani wenye ujuzi wa hali ya juu katika kazi zao.

"Tunataka ifike wakati vyuo vyetu vinazalisha wataalamu wenye ujuzi wa hali ya juu ili kuendena na soko la ajira nchini, isiwe mhitimu anakuwa na elimu ya darasani huku nadharia inamshinda," alisema.

Alisema kuwa ili kufikia malengo hayo serikali imevipatia vitendea kazi baadhi ya vyuo vya serikali na binafsi ili kuhakikisha malengo hayo yanakamilika.

"Kuna vyuo tumevipatia matrekta kwa ajili ya kilimo pamoja na kuhakikisha kila chuo kinakuwa na mashamba makubwa ya wanafunzi na wananchi kujifunza," alisema.

Alisema serikali ina vijengea vyuo vyake uwezo wa kujitegemea kwenye bajeti zao na kuacha kulalamika kuhusu matatizo ya fedha kila siku.

"Serikali tunataka kiongozi unapotembelea chuo unapewa mipango mikakati ya maendeleo kutokana na chuo kuwa na uwezo wa fedha za kujiendesha sio kulalamika kuwa kuna matatizo ya kifedha huko," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza la Ujuzi la Kilimo (ASSC), Fabian Mwakatuma, alisema baraza hilo lilianzishwa Juni 2019 kwa nia ya kusaidiana na serikali kukabiliana na matatizo kwenye sekta ya kilimo nchini.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## TANGAZO KWA UMMA

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inawaalika mafundi umeme wote wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwenye semina ya siku tatu (3) itakayoanza saa tatu (3) asubuhi, tarehe **30/09/2020** hadi tarehe **02/10/2020.** Semina itafanyikia ukumbi wa Baraza la **Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)** uliopo Mikocheni eneo la Viwanda.

Baadhi ya mambo yatakayofundishwa ni pamoja na namna ya kupima vitu muhimu kama vile earth resistance, insulation resistance na earth loop impedance katika mfumo wa umeme.

**Jinsi ya kufika ukumbini:** ***kutokea Kituo cha basi ITV, fuata barabara inayokwenda Chuo cha Kodi Mikocheni, elekea upande wa kulia.***

Kwa mafundi watakaopenda kuhudhuria wathibitishe ushiriki wao kabla ya tarehe 29/09/2020 kwa kupiga simu au kutuma ujumbe mfupi **(SMS) 0754 26 59 36 au piga +255222123850/3/4/6.**

**MAFUNZO HAYA NI BURE KABISA**

**Limetolewa na**

**MKURUGENZI MKUU**
**EWURA**

215915402

# Mbwa wazururaji 280 wapigwa risasi

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imeendesha msako wa kuua mbwa wanaozurura mitaa mbalimbali bila kuwa na ulinzi, ambapo mbwa 280 kati ya 300 wameuliwa kwa kupigwa risasi.

Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Jiji hilo, Gration Mwesiga, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu msako huo.

Mwesiga alisema waliandaa risasi 300 kwa ajili ya kuua mbwa idadi hiyo, lakini walifanikiwa kuua 280, ili kuwadhibiti wasisababishe madhara kwa binadamu.

Pia alisema wametoa chanjo 502 kwa mbwa wanaofugwa.

"Bado tunaendelea na zoezi la kuua mbwa wazururaji, lengo ni kuepusha kuwasababishia binadamu kichaa cha mbwa wanapong'atwa," alisema.

Alisema, Jiji hilo limejipanga kutokomeza mbwa hao, na kwamba wanataka kuona kila mbwa anayeonekana mtaani anakuwa na makazi maalum.

Aliwataka wananchi wa maeneo mbalimbali kutoa taarifa pale wanapoona kuna mbwa wanazurura na hawana wamiliki, ili wawateketeze kuepuka kuleta madhara kwa jamii.

"Tunapita kila kona maana wapo wengi wanazurura," alisema.

Kuhusu chanjo, alisema wanaendelea, pia kutoa chanjo kwenye maeneo mbalimbali.



Baadhi ya wanafunzi wa darasa la saba wa Shule ya Msingi St. Veritas ya Kimara, jijini Dar es Salaam, wakipongezwa na walimu wao, katika mahafali iliyofanyika kabla ya kufanya mtihani wa taifa mwezi ujao. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TCRA yakilima faini kituo cha redio

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imeitoza faini ya Sh. milioni tano Redio Ihsaan ya mkoani Tanga kwa kosa la kukiuka kanuni za mawasiliano ya kielektroniki na posta.

Sambamba na hilo, kituo hicho kimepewa onyo na kutakiwa kuomba radhi kwa wasikilizaji wake kwa siku tatu mfululizo kupitia kipindi cha Al Jawaabul Kaafi.

Akitangaza uamuzi wa Kamati ya Maudhui TCRA jijini Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Joseph Mapunda, alisema kupitia kipindi cha Al Jawaabul Kaafi, kituo hicho kilirusha maudhui yenye lugha ya matusi, kashfa na isiyokuwa na staha mbele ya jamii.

Mapunda alisema watangazaji walimruhusu Sheikh Salim Barahiyan, kujibu maswali ya wasikilizaji huku watangazaji wakichombeza na kuonyesha kufurahia maneno yake.

Alisema uamuzi huo wa TCRA ni kwa mujibu wa Kifungu cha 28 (1) (b) na (d) cha Sheria ya Mamlaka hiyo, Sura ya 172 marejeo ya mwaka 2017.

"Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na uongozi wa Radio Ihsaan, kamati imeridhika kuwa wamekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) ya mwaka 2018 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Gazeti la Serikali Na.486 ya 2020," alisema Mapunda.

Alisema kwa mujibu wa leseni, redio hiyo ilitakiwa kutoa huduma ya maudhui, kuhakikisha inazingatia sheria, kanuni na masharti ya leseni wakati wote wa utoaji huduma.

"Kwa marekebisho yaliyofanyika mwaka huu, sheria inamtaka kila mwenye leseni ya utoaji huduma ya maudhui kuhakikisha hatoi maudhui yasiyostahili muda ambao idadi kubwa ya watoto inaweza kuwa sehemu ya hadhira yake," alisema Mapunda.

Alisema kwa kanuni hiyo hiyo, inamtaka kila mwenye leseni ya utoaji huduma kuhakikisha hatoi maudhui ambayo yanaonyesha vurugu, unyanyasaji wa kijinsia, mwenendo dhahiri wa kingono au lugha ya kukera inayokusudiwa kipindi cha watu wazima.

Aliongeza kuwa Kanuni Na: 11, kanuni ndogo ya kwanza, ya pili (b) ya kanuni za mawasiliano ya kielektroniki na posta ya 2018, inakataza mtoa huduma ya maudhui kutangaza masuala ya ngono kwa njia ya wazi na kukera.

Alisema faini hiyo inapaswa kulipwa ndani ya siku 30 tangu kusomwa kwa hukumu hiyo.

Alisema, kukata rufani dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki za Kibiashara (FCT) iko wazi ndani ya siku 21

# Bili maji Zanzibar kulipwa kidijitali

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA wa Zantel sasa wanaweza kulipia bili za maji kiurahisi zaidi kwa njia ya Ezypesa baada ya kampuni hiyo kuingia ubia na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), mfumo wa kidigitali zaidi wa kufanya malipo.

Hatua hiyo itaongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato huku ikiwapunguzia wateja, adha ya kusafiri umbali mrefu, ili kulipia huduma hiyo muhimu.

Akizungumza juzi wakati wa hafla ya uzinduzi huo, Mkurugenzi Mkuu wa Zawa, Mussa Ramadhan, alipongeza hatua hiyo akieleza kuwa, itasaida katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja visiwani Zanzibar.

"Mkakati wetu ni kuendeleza na kutoa huduma ya maji ya uhakika na nafuu kwa wateja wetu, hivyo ushirikiano wetu na Ezypesa utasaidia katika kufikia malengo yetu kwani utaongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kuwapunguzia wateja mzigo wa kutembea umbali mrefu kwani kwa sasa kila kitu kitafanyika kwa simu," alisema.

Ramadhani alisema huduma hiyo ni suluhisho katika kuongeza kasi na ufanisi wa ukusanyaji wa mapato hivyo kusaidia mamlaka kuwa na uwezo wa kuboresha miundimbinu ya maji na kuwafikia watu wengi zaidi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Zantel-Zanzibar, Khamis Mussa, alisema hatua hiyo ni muhimu katika kutekeleza mkakati wa Zantel wa kuboresha maisha ya watu kupitia huduma za Ezypesa, ambazo zinawapa wateja wake uhuru na urahisi wa kupata huduma mbalimbali.

"Kupitia Ezypesa tumejizatiti katika kuboresha maisha ya watu kwenye nyanja mbalimbali, ili kuwezesha urahisi wa upatikanaji wa huduma na mahitaji ya kila siku. Ushirikiano wetu na ZAWA ni hatua muhimu katika kuhakikisha wateja wetu wanalipia ankara za maji mahali popote," alisema Mussa.

"Tofauti na njia za awali, kwa sasa hakuna haja tena ya kutembea umbali mrefu, ili kulipia bili au kusubiri mpaka maji yakatike kwa kuchelewesha bili, kwa simu yako tu unaweza kujihakikisha unapata huduma ya maji," aliongeza.

Alisema ni dhahiri kuwa maji ni rasilimali muhimu katika kuchochea huduma za kibiashara pamoja na zile za majumbani na mamlaka ya maji Zanzibar (ZAWA) inafanya jitihada kubwa kusimamia huduma ambayo hadi sasa imewafikia wateja 1,161,915 visiwani Zanzibar.

# CHUO CHA VETA CHA MAFUNZO YA HOTELI NA UTALII (VETA HOTEL AND TOURISM TRAINING INSTITUTE) VHTTI




## 1. IJUE TAASISI YA VHTTI

VHTTI ni Chuo cha Serikali kinachomilikiwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.
Chuo hiki kilianzishwa rasmi mwaka 2010, kikiwa na lengo kuu la kuandaa rasilimali watu katika kada ya kati katika tasnia ya Hoteli na Utalii. Chuo kimesajiliwa na kupata ithibati ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kwa namba ya usajili REG/BTP/001 mapema mwaka 2013, inayokipa chuo mamlaka ya kutoa mafunzo ya programu za NTA kuanzia ngazi ya cheti cha awali cha ufundi mchundo NTA4 hadi ngazi ya Diploma NTA6 katika sekta ya hoteli na utalii.

Chuo cha VETA cha Mafunzo ya Hoteli na Utalii kipo jijini Arusha katika eneo maarufu la Njiro takribani kilomita 13 kutoka katikati ya mji wa Arusha. Taasisi hii ipo jirani na Taasisi nyingine maafuru kama Tume ya Mionzi Tanzania (TAEC), Taasisi ya Uhasibu ya Arusha (IAA) na Taasisi ya Uongozi ya Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAMI).

Chuo cha VETA cha Mafunzo ya Hoteli na Utalii kipo Arusha kimkakati kwa kuwa Arusha ipo kwenye kitovu cha ukanda wa Utalii wa Kaskazini mwa Tanzania (Northern Tourism Circuit). Hii imeiweka Taasisi jirani sana na wadau muhimu wa Hoteli na Utalii, hivyo kurahisisha utoaji wa mafunzo stahiki.

## 2. SHUGHULI ZINAZOFANYWA NA CHUO CHA VETA CHA MAFUNZO YA HOTELI NA UTALII

Chuo kinafanya shughuli kuu nne ambazo ni pamoja na:

i. Kuendesha mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika nyanja za Hoteli na Utalii NVA Level 1-3 na NTA Level 4-6).
ii. Kutoa huduma ya Hoteli kupitia Hoteli yake ya mazoezi yenye hadhi ya nyota tatu.
iii. Kutoa ushauri elekezi katika mambo mbalimbali ya Hoteli na Utalii.
iv. Kufanya tafiti zinazochangia maendeleo katika sekta ya Hoteli na Utalii.



*Mwanafunzi wa fani ya mapishi akiwa ameandaa kitindamio(Dessert) katika hoteli ya VHTTI*

## 3. MAFUNZO YANAYOTOLEWA NA VHTTI

Mafunzo yanayotolewa yako katika programu kuu mbili ambazo ni:

a) Programu zenye ithibati ya VETA -Daraja la 1-3 (NVA 1-3).
b) Programu zenye ithibati ya Baraza la Mafunzo ya Ufundi (NACTE)- Daraja la 4-6 (NTA 4-6).

**Programu zenye usajili na ithibati ya VETA za NVA I-III**

Kuanzia mwaka wa masomo wa 2018/2019 Chuo kilianza rasmi kutoa mafunzo ya muda mrefu yenye ithibati ya VETA.



*Mwanafunzi wa kozi ya mapokezi akiwa anapokea wageni katika hotel ya VHTTI , Njiro*

Katika Programu kuu tano ngazi za VETA (National Vocational Award) Level I, II & III kwa miaka miwili kama ifuatavyo:

i. Mafunzo ya Mapishi (Food Production).
ii. Mafunzo ya mapokezi ya wageni (Front Office Operations)
iii. Mafunzo ya Huduma na Mauzo ya vyakula na vinywaji (Food and Beverage Service and Sales).
iv. Mafunzo ya usafi na unadhifu wa vyumba, wageni, mazingira na huduma za udobi (Housekeeping and Laundry Services).
v. Mafunzo ya Uongozaji Watalii (Tour Guide).

**Sifa za kujiunga kwa program hizi za NVA ni:**

- Ufaulu wa mtihani wa kidato cha nne kwa anga¬lau masomo mawili kwa kiwango chini cha alama 'D" au zaidi.

## 4. PROGRAMU ZENYE ITHIBATI YA NACTE

Chuo cha VETA cha Mafunzo ya Hoteli na Utalii kilipata usajili wa kudumu na ithibati ya NACTE tangu mwaka 2013. Tangu wakati huo kinaendesha Programu zinazotambuliwa na Baraza la Ufundi la Taifa katika ngazi za NACTE. National Technical Award (NTA) Level 4, 5 na 6. Programu zinazotolewa katika ngazi hizo ni:

i. Culinary Arts (Sanaa ya Uandaaji na Upishi wa Chakula)
ii. Food and Beverage Service and Sales (Uhudumu na Uuzaji wa vyakula na Vinywaji)
iii. Rooms Division (Mapokezi na utoaji wa huduma ya malazi kwa wageni).
iv. Tour Guiding (Uongozaji Watalii).
v. Travel and Tour Operations (utaalamu wa kutafuta, kupanga na kusimamia safari za Watalii).

## 5. MIUNDOMBINU YA KUFUNDISHIA

VHTTI ina mazingira rafiki na miundo mbinu inayomwezesha mwanafunzi kupata umahiri katika Nyanja ya Hoteli na Utalii. Miundo mbinu inajumuisha mambo sita kama ifuatavyo:

i. Hoteli ya mazoezi ya kisasa yenye vyumba 25. Hoteli hii yenye hadhi ya nyota tatu (3) inatoa huduma kwa wateja kama zilivyo hoteli nyingine kwenye soko la ajira. Hii ni Hoteli ya mazoezi kwa kuwa hutumika kuwaandaa wanafunzi kwa mazingira halisi ya soko la ajira. VHTTI ndiyo chuo pekee kinachotoa mafunzo ya hoteli nchini chenye hoteli yenye ubora uliothibitishwa na Wizara ya Mali Asili na Utalii.
ii. VHTTI ina karakana (workshop zenye vifaa vya kisasa kwa kila Programu) Mazingira ya elimu kwa vitendo yanahusisha 'simulation restaurant and bar, demonstration kitchen, application kitchen, butcher, laundry facility, camping kitchen tent, sleeping tents, sleeping bags, Tour Guiding Gadgets (binoculars, cameras and GPS)".
iii. VHTTI ina madarasa ya kutosha yenye kutoa nafasi rafiki kwa kufundishia na kujifunzia. Madarasa na karakana hutumiwa na wanafunzi wa mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

# TOLEO MAALUM

iv. VHTTI inatoa malazi yenye ubora na huduma ya chakula kwa wanafunzi inayoendana na fani ya ukarimu. Makazi ya wanafunzi ni nadhifu na yenye kukidhi mahitaji ya kiafya kwa jinsia zote.
v. Chuo kina mazingira tulivu na mazuri kwa kujisomea.
vi. Chuo pia kina miundombinu ya mtaala wa ziada (Extra curricula activities) kama michezo, utamaduni na sanaa. Hii inashamirishwa na viwanja vya mpira wa kikapu, wavu, mpira wa miguu, kumbi, bwawa la kuogelea na michezo mingine.

**6. MAFUNZO KWA VITENDO**

Ili kutoa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko la ajira VHTTI imeyapa mafunzo ya vitendo kipaumbele stahiki. Mafunzo ya vitendo huchukua takiribani 70% ya mafunzo yote yatolewayo na chuo. Njia kuu za kutolea mafunzo kwa vitendo ni kama zifuatavyo:

i. Mafunzo yatolewayo na walimu katika karakana (practical workshops) za chuo
ii. Mafunzo yatolewayo kupitia masaa ya kujifunza kwa vitendo (Application Hotel contact hours) katika hoteli ya mazoezi ya chuo.
iii. Mafunzo kwa vitendo yanayotolewa na hoteli au kampuni za utalii marafiki zilizo jijini Arusha wakati wa 'orientation prorammes, day release arrangements and casual labor support".
iv. Mafunzo maalumu ya vitendo ya mahali pa kazi (Industrial Training Programme) yanayotolewa kama sehemu ya mwisho wa utahini wa ujuzi kwa vitendo. Mafunzo haya hufanyika katika hotel/lodges na makampuni ya utalii yaliyopo nchini.

**7. USHIRIKIANO NA WADAU WA NDANI NA NJE YA NCHI**


Ili kufanikisha utoaji wa mafunzo stahiki na kwa namna inayokidhi viwango, VHTTI imehakikisha uwepo wa ushirikiano madhubuti na wadau mbalimbali. Baadhi ya wadau wake wakuu ni:

i. Mamlaka za Ithibati (Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi-NACTE-NTA 4, 5 na 6 na VETA-NVA LEVEL I-III)
ii. Chama cha Wenye Hoteli (Hotel Association of Tanzania)
iii. Chama cha wenye Kampuni za Utalii ( Tanzania Association of Tour Operators)
iv. Chama cha Waongoza Utalii (Tanzania Tour Guide Association)
v. Chama cha Waongoza Watalii Wapanda Mlima Kilimanjaro na Meru (Kilimanjaro Mountain Guide).
vi. Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (Ngorongoro Conservation Authority)
vii. Mamlaka ya Mbuga za Wanyama (Tanzania Tanzania National Parks Authority)
viii. Mamlaka ya Hifadhi ya Mlima Kilimajaro (Kilimanjaro National Park Authority).

**8. MAFANIKIO**

Ndani ya kipindi cha miaka tisa ya utoaji mafunzo, VHTTI kupitia ushirikiano madhubuti na wadau wake imeweza kuwa kinara katika kuandaa na kutoa wahitimu wenye umahiri unaotakiwa kwenye soko la ajira. Wengi wa wahitimu wa VHTTI wanafanya kazi katika hoteli, mamlaka za uhifadhi za serikali, makampuni binafsi ya waongoza watalii na lodges zenye hadhi ya juu na katika nyadhifa za usimamizi. Wengine wengi wameweza kujiajiri na kutengeneza ajira kwa watanzania wenzao. Lakini pia, mafanikio katika umahiri wa wanafunzi wetu unabainishwa na mrejesho ambao chuo kinaupata kutoka kwa viongozi wa hoteli/lodges, mamlaka za uhifadhi, na makampuni ya waongoza watalii ambako wanafunzi wetu hufanya mazoezi ya vitendo.

VHTTI imeweza kuitunza hoteli yake ya mazoezi kitaalamu na kuifanya kuwa na hadhi ya nyota tatu. Hadhi hii inatokana na uchunguzi uliofanywa na Wizara ya Utalii na Maliasili mwaka 2017.



Jengo la hoteli "Application Hoteli" inayotumika kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa wanachuo wa VHTTI

Sifa ya VHTTI imeanza kupenya hata nje ya mipaka ya Tanzania kwa kuvutia wanafunzi kutoka mataifa jirani. Mataifa ambayo raia wake wanasoma au wamehitimu mafunzo hapa chuoni ni pamoja na: Uganda, Kenya, Zambia na Zimbabwe.



Wanafunzi wa kozi ya uongoza utalii (Tour Guiding) wakifunga Hema linalotumika kama malazi kwa watalii

VHTTI kwa kushirikiana na chuo cha Canada cha Nova Scotia Community College (NSCC) imeanzisha kozi mpya za Tour Guiding na Travel and Tour Operations. Kozi hizi mbili ni matokeo ya utafiti wa soko la ajira uliofanyika mwa 2017 unaoratibiwa na VETA. Pia kwa ushirikiano huo tumeanzisha mafunzo ya muda mfupi yanayoshirikisha wanafunzi wa Canada na VHTTI katika Programu za 'Oral history and Cultural Tourism, Entrepreneurship, Exceeding Customer Expectations na Managing a Winning Team".

Chuo kimefanikiwa kujenga uwezo wa watumishi wake hususani walimu katika nyanja za hoteli na utalii na njia bora za ufundishaji. Sehemu kubwa ya mafunzo yamefanyika nchini Canada ambapo jumla ya walimu kumi na moja (11) wamepokea mafunzo hayo kati ya mwaka 2015 na 2017.

**9. NAFASI ZA MASOMO KWA MWAKA WA MASOMO 2020/2021**

Mkuu wa Chuo cha VETA cha Mafunzo ya Hoteli na Utalii anawatangazia nafasi za Masomo kwa mwaka wa masomo 2020/2021 kwa ngazi ya Astasha¬hada (Certificate) na Stashahada (Diploma), katika fani za hoteli na utalii kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| i. Culinary Arts (CA) | - | Level 4,5 & 6 |
| ii. Rooms Division (RD) | - | Level 4,5 & 6 |
| iii. Food and Beverage Service and Sales (FBSS) | - | Level 4,5 & 6 |
| iv. Tour Guide (TG) | - | Level 4 |
| v. Travel and Tour Operations (TTO) | - | Level 5 & 6 |

**SIFA ZA KUJIUNGA NA PROGRAMU ZA NTA NI KAMA IFUATAVYO:**

**Cheti cha Msingi (Basic Technician Certificate-NTA level 4)**

- Ufaulu wa mtihani wa kidato cha nne kwa anga¬lau masomo manne kwa kiwango cha alama 'D" AU
- Cheti cha kidato cha nne chenye walau pass mbili (2) na Cheti kinachotambuliwa na VETA cha NVA level 3.

**Cheti cha Ufundi Sanifu (Technician Cer¬tificate-NTA level 5)**

- Ufaulu wa mtihani wa kidato cha nne kwa anga¬lau masomo manne kwa kiwango cha alama 'D" na Cheti cha Msingi (NTA level 4) kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) AU
- Ufaulu wa mtihani wa kidato cha sita angalau somo moja katika kiwango cha alama E (Principal pass) na somo moja alama S (Subsidiary pass). AU
- Cheti cha kidato cha nne chenye walau pass nne (4) na Cheti kinachotambuliwa na VETA cha NVA level 3.

**Cheti cha Diploma (Ordinary Diploma-NTA level 6)**

- Ufaulu wa mtihani wa kidato cha nne kwa anga¬lau masomo manne kwa kiwango cha alama 'D" na Cheti cha ufundi Sanifu (NTA level 5) kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) AU
- Ufaulu wa mtihani wa kidato cha sita angalau somo moja katika kiwango cha alama E (Principal pass) na somo moja alama S (Subsidiary pass) na Cheti cha ufundi Sanifu (NTA level 5) kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE).

Maombi kwa Programu zote yameanza kupokelewa kuanzia **tarehe 15 Juni 2020.** Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **15 Septemba, 2020.** Maombi yatumwe kwa Mkuu wa Chuo, fomu zinapatikana chuoni – VHTTI. Ada ya maombi ni **TSh.10, 000/=**

**WAHI MAPEMA KWANI NAFASI NI CHACHE NA ADA ZETU NI NAFUU SANA.**

**KUMBUKA: NAFASI ZA HOSTELI ZINAPATIKANA KWA WATAKAOWAHI.**

**Kwa mawasiliano zaidi**
**Email: vhtti@veta.go.tz au info.vhtti@gmail.com**
**Namba za Simu +255 (027) 297 00096 au 0715782232**

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 29, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12
FUNZO COVID- 19



Ukurasa 13
**Nganza ilivyotesa tuzo wanasayansi chipukizi**



Ukurasa 14
Kahama yawa kipaumbele elimu na ulinzi wa wazee

TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU

# MAGEUZI JIKONI

• Ni jiko mbadala gesi, mkaa, kuni • Kwa 175/- kilo ya maharage huiva

KUPIKA chakula iwe nyumbani, migahawani na kwenye jumuiya zenye walaji wengi kama vyuoni na shuleni ni changamoto kutokana na ugumu na upatikanaji wa nishati ya uhakika.

Chanzo kikuu cha nishati ya kupikia ni kuni au mkaa ambavyo vina athari kubwa kwenye mazingira inayotokana na kukata misitu, kuchafua hewa na kuongeza joto duniani, kuchagiza ukame, uhaba wa maji na magonjwa hasa ya mfumo wa hewa na kifua.

Utafiti wa hivi karibuni uliofanywa na taasisi ya kuendeleza huduma za nishati endelevu (TaTEDO) kwa kushirikiana na kampuni ya Gamos pamoja na vyuo vikuu vya Surrey na Loughbrough vya Uingereza unaonyesha kuwa teknolojia imewezesha kupata vifaa vya kupikia vyenye ufanisi.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa TaTEDO, Estomiah Sawe, anasema na kuvitaja kuwa ni pamoja na jiko sanifu la umeme lenye presha (JULEP) ambalo linatoa fursa ya kuunganisha juhudi za kusambaza umeme, kutumia kuwasha taa na kupikia kwa gharama ndogo.

"Kutegemeana na chanzo, matumizi ya umeme kupikia kwa kutumia JULEP sasa yanatambuliwa kuwa ndiyo suluhisho sahihi na endelevu la nishati ya kupikia hapa nchini," anasema.

Sawe anasema kwa kutumia JULEP na vifaa vingine sanifu, kaya zenye umeme zinaweza kutumia kupika kwa gharama nafuu kuliko kutegemea mkaa na gesi.

Anaeleza kuwa ni jiko linalopika kwa kutumia joto na presha ya mvuke unaokusanywa ndani ya sufuria, nishati inayotumika ni kidogo sana kuivisha chakula kwa muda mfupi na kuhifadhi ladha, hivyo huokoa fedha, muda, afya na mazingira.

Aidha, linaweza kupika kwa kuchemsha, kuoka, kukaanga na kuunga na hujumuisha vifaa vya kupikia kama kasha la kuhifadhi joto, jiko la umeme pamoja na sufuria, anaongeza Sawe.



Kinamama wajasiriamali wanufaika na mafunzo ya matumizi ya majiko sanifu ya umeme yanayotumia nishati kidogo kuivisha vyakula kwa muda mfupi. **PICHA: MWANDISHI WETU**

### FAIDA ZA JULEP

Akizungumzia zaidi faida Sawe anasema utafiti huo pia unadhihirisha kuwa kupika kwa mkaa hutumia nishati nyingi mara 5.5 zaidi ya kupika kwa gesi na mara 13 zaidi ya kupika kwa umeme kwa kutumia jiko sanifu la umeme lenye presha.

Ukiwa na vifaa sanifu vya kupikia kama jiko sanifu la umeme lenye presha (JULEP), utaweza kupika kwa chini ya uniti 2 za umeme kwa siku sawa na 720/- kwa watumiaji wa umeme wa gridi ya taifa. Mbinu za kupika zinaweza kuwa ni kichocheo kikubwa katika matumizi sanifu ya nishati na hivyo kupunguza matumizi ya umeme hadi uniti moja kwa siku. Kwa familia ya kawaida watu watano mpaka nane, wastani wa gharama ya kupika vyakula vyote kwa jiko sanifu la umeme lenye presha ni Sh. 21,900 kwa mwezi. Anaeleza kuwa chakula kilichopikwa kwenye jiko sanifu la umeme lenye presha kina ladha bora zaidi kuliko kilichopikwa kwenye gesi na mkaa.

Sawa anaeleza kuwa jiko la JULEP linatunza virutubisho vya chakula na lina uwezo wa kupika vyakula mbalimbali iwe kwa kuchemsha au kurosti, kuunga na kukaanga huku likitumia umeme kidogo sana mfano kilo moja ya maharage inapikwa kwa nusu uniti (sawa na Shilingi 140 mpaka 175).

Aidha, anasema linaokoa nishati kwa asilimia 85, muda na fedha na ni salama kwa mtumiaji.

### USAMBAZAJI TEKNOLOJIA

Ili usambazaji wa JULEP uenee sehemu kubwa ya nchi, kunahitajika kuwapo na sera wezeshi, uwekezaji kwenye teknolojia hiyo na ushirikiano kwenye sekta mbalimbali zinazohusika na nishati. Kwa sasa hivi kuwapo umeme na kuutumia kupikia vinaonekana kama vitu viwili visivyowezekana, anasema Sawe.

Anafafanua kuwa ili watu wengi waweze kupata teknolojia hii, mambo ya lazima yanayotakiwa kufanyika ni pamoja na kuhamasisha wajasiriamali kuagiza majiko sanifu ya umeme yenye presha kwa wingi.

Aidha, kupunguza au kuondoa kodi na kuhakikisha ubora wa bidhaa hizo kwa wateja na pia soko likikua, kujenga kiwanda hapa nchini cha kuyazalisha majiko hayo kwa kutumia kampuni za wananchi wenyewe na kuendeleza soko na mitandao kwa ajili ya kuyasambaza na kutoa huduma kwa wateja kama pembejeo, ufundi na kuwawezesha wajasiriamali.

Kadhalika Sawe anaongeza kuwa inatakiwa kuwasaidia wateja ili waweze kuyanunua kwa kuweka njia mbalimbali, ili yatumike kupika vyakula wanavyopenda kwa kuzielewa faida zake.

### INAHITAJIKA KASI ZAIDI

Meneja wa kampuni ya Sustainable Energy Enterprise Ltd, Shima Sago, anasema kuwa soko rasmi la nishati ya kupikia kwa Tanzania halijaendelezwa na limeshikiliwa na kuni na mkaa.

Serikali imejiwekea lengo la muda mrefu kuhakikisha zaidi ya asilimia 75 ya kaya zote nchini zinatumia nishati na teknolojia za kisasa kupikia ifikapo mwaka 2030. Katika eneo hilo msukumo upo kwenye gesi ya mitungi (LPG), bayogesi, umeme na majiko sanifu.

Hata hivyo, Sago anasema hakujawa na matokeo ya kuridhisha, akitolea mfano anasema kuwa bayogesi bado haijaweza kutumiwa na wananchi wengi kutokana na gharama za awali za kutengeneza mtambo kuwa kubwa na changamoto ya kuhudumia kila siku.

Pia majiko ya kawaida ya umeme yalizoeeleka, gharama za kuyanunulia pamoja na bili za umeme kubwa, zimefanya wananchi wengi wasipikie umeme.

Adha, juhudi chache zimefanyika kukuza matumizi ya majiko

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# FUNZO COVID- 19

• Wanawake wabaki na ngeu
• Yaleta utii sheria bila shuruti

KIPINDI cha COVID-19 katika miaka ya hivi karibuni ndiyo wakati uliochia dunia 'makovu na ngeu' za kiafya, kiuchumi na hata kisaikolojia.

Kwa Tanzania msimu wa kuanzia Machi mwaka huu ulikuwa ujio wa corona. Jamii ilipata funzo na huo ukawa mwanzo wa kuujua umuhimu wa kufuatilia vyombo vya habari, kufuata maelekezo ya kitaalamu na maagizo ya serikali kukabiliana na COVID-19, lakini kijifunza kuweka akiba.

Ahueni ilionekana Juni, mwaka huu, Rais John Magufuli, alipotangaza shughuli za kiuchumi na kielimu kuendelea ikiwamo kufungua vyuo vikuu na shule za sekondari na msingi zilizofungwa tangu Machi kuepusha maambukizi.

Aidha, watu waliruhusiwa kuendelea na shughuli zao kama kawaida, hatua iliyokuwa mkombozi kwa makundi maalum ndani ya jamii, hususani wasichana na wanawake ambao waliathiriwa zaidi.



Kunawa na maji tiririka kunasaidia kujikinga na corona, liwe jambo endelevu ili watu wajiepushe na maradhi ya kuambukizwa yanayotokana na kula au kugusa. **PICHA: MTANDAO**

### UKATILI NA CORONA

Katika semina za jinsia na maendeleo ngazi ya jamii (GDSS) zinazoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), zikishirikisha wadau mbalimbali, washiriki wanaelezea funzo walilopata katika kipindi hicho.

Agness Lukanga, mmoja wa wawezeshaji wa semina hizo zinazofanyika Dar es Salaam, akizungumza mada kuhusu, 'madhara ya ukatili wa kijinsia uliosababishwa na janga la corona kwa wanawake na watoto wa kike', anasema zipo athari chanya na hasi katika kipindi hicho.

Anasema, inafahamika kuwa corona ilileta madhara mengi kwa wanawake na watoto pamoja na mzigo wa majukumu kwa mama kuongezeka, huku baadhi ya wanaume kuacha majukumu.

Anaongeza kuwa kulikuwa na taarifa za wanawake na wasichana, kubakwa na kusababisha mimba za utotoni, uzururaji kwa watoto pamoja na vipigo na ukatili kwa watoto.

Anasema serikali na asasi zisizo za kiserikali ziweke mikakati madhubuti kuhakikisha kuwa majanga hayaongezi mzigo wa majukumu kwa wanawake na wasichana.

> Mfano katika suala la kunawa mikono, ilikuwa ni utaratibu, mtu kabla hajahudumiwa alinawa ili aingie dukani.

Lukanga anasema ipo haja ya kuongeza hamasa ya wanawake kuendelea kuinuka kiuchumi na kujenga mazoea ya kukabiliana na changamoto zinazoibuka.

"Corona ilidumaza watu kibiashara hasa wanawake, kwa nchi za Afrika, hivyo inatakiwa kutambua namna ya kujiandaa kisaikolojia na na jinsi ya kujipanga iwapo yatatokea majanga kama hayo duniani," anasema Lukanga.

"Kama serikali ilivyotoa vipindi vya masomo ya shuleni kwenye redio na runinga pia itoe vipindi vya elimu kuhusu ukatili wa kijinsia kipindi cha majanga. Mimba za utotoni kwa wasichana zipatiwe ufumbuzi, pamoja na mambo mengine elimu na nguvu za pamoja zinahitajika," anasema Lukanga.

### MWAMKO KISHERIA

Washiriki wa semina hizo, akiwamo Anna Mfaume kutoka Kitunda Dar es Salaam, anasema katika kipindi cha corona, anasema jamii inaweza kutii sheria na kanuni bila shuruti na hilo lilionekana wakati wa corona.

"Mfano katika suala la kunawa mikono, ilikuwa ni utaratibu, mtu kabla hajahudumiwa alinawa ili aingie dukani. Kwenye daladala levo siti ilikuwa kawaida. Watu walikuwa wakiona basi limejaa walipopanda walishuka wenyewe, hata kondakta alikuwa mmoja bila mpigadebe," anasema Anna.

Anaungwa mkono na mshiriki Aloyce Anthony, anayesema utamaduni wa kufuata kanuni za kiafya ikiwamo kunawa mikono iwe ni utaratibu wa kudumu.

"Kipindi cha corona kilionyesha namna watu wanavyoweza kuheshimu kanuni na taratibu, ilikuwa kila biashara, nyumba na maeneo ya taasisi za umma na binafsi utaratibu wa kunawa kabla ya kupatiwa huduma, hii ilipunguza magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu," anasema Anthony.

Mshiriki mwingine kutoka Mabibo, Hamida Mbwana, anasema kipindi hicho, kilipunguza matukio ya kuwapuuza wanawake na kuzichukia familia kwa baadhi ya wana jamii hususani wanandoa.

"Ilikuwa wakinababa, hao waume zetu walitumia muda mwingi nyumbani na familia zao, tofauti na kipindi kingine mwanaume alirudi usiku sana na hakuwa na wakati wa kutatua changamoto za familia na ulikuwa mzigo kwa mwanamke anayeshinda nyumbani kutwa na familia yake." Anasema Hamida.

Mshiriki mwingine kutoka Manzese, Kennedy Macher anasema, harakati za wanawake katika shughuli za kiuchumi na kisiasa zilikumbwa na changamoto nyingi akisema mikakati ya kujiandaa na mwaka wa uchaguzi 2020, kuleta mabadiliko ya uongozi kisiasa, unaweza kuathirika pia kutokana na corona.

Aasema pamoja na athari hizo, zipo changamoto walizokumbana nazo wanawake na wasichana kwa kukumbana na ukatili wa kijinsia.

"Mwaka wa uchaguzi kama miaka mingine, ni kawaida kuwa na maandalizi ya ndani kwa taasisi kuandaa kundi maalumu la wanawake wagombea, kuwapa mbinu za namna ya kujipanga kukabiliana na ushindani katika siasa, ili wajiamini na kutoa hamasa kwa viongozi wanawake watarajiwa," anasema Machery.

Anabainisha kwamba athari za maandalizi duni kwa kundi hilo zinaweza kurudisha nyuma azma ya wanasiasa, wanawake wanaoibukia sasa.

"Kipindi hicho baadhi ya wanawake familia zao zilikumbwa na changamoto za kiuchumi na kusababisha baadhi kusambaratika," anasema.

## MAGEUZI JIKONI

**INATOKA UK.11**

sanifu ya kuni na mkaa, inaeleweka kuwa hizo ni hatua za mpito tu na sio za muda mrefu."

Meneja wa Sustainable Energy Enterprise, anaongeza kuwa kutegemea kuni na mkaa kutaendelea kupungua kutokuwa endelevu katika kipindi cha muda mrefu kutokana na ongezeko la watu ambalo linaweka mzigo mkubwa kwenye misitu.

"Inafahamika kuwa gesi ya mitungi au LPG, tunayoitumia inatokana na mafuta na huagizwa nje, siyo endelevu kwa kipindi cha muda mrefu. Pamoja na kuwa siyo endelevu, pia inaweza si ya kuaminika kutokana na kuwa inaagizwa kutoka nje". Sago anasema inategemea soko la mafuta na hakuna udhibiti wa bei na hata upatikanaji wake, hivyo kufanya kuwepo uwezekano wa watumiaji kurudi kutumia kuni na mkaa pale itakapokuwa haipatikani au bei kupanda.

Hivyo, gesi nayo inaoenekana kuwa nishati ya mpito badala ya suluhisho la kudumu na la muda mrefu.

Tanzania inatumia fedha nyingi za kigeni kuagiza gesi ya LPG kutoka nje japo inayo gesi asilia na juhudi zinaendelea kukuza matumizi yake hapa nchini.

Hata hivyo, kama ilivyo gesi ya LPG ya asilia siyo endelevu kwa kuwa baada ya kipindi itakwisha na pia kwa kiwango inachangia hewa ya ukaa.

Wadau wa nishati wanaona kuwa kutokana na changamoto hizo upo umuhimu kwa taifa kutafuta na kutumia nishati na teknolojia ambayo ni ya uhakika, nafuu na yenye uendelevu wa muda mrefu tofauti na nishati zilizotajwa hapo juu .

SAYANSI

CRISPIN GERALD NA
ELIZABETH ZAYA

# Nganza ilivyotesa tuzo wanasayansi chipukizi

## • Wagundua lishe 'bomba' mseto samadi, nafaka

JITIHADI za kuwaibua na kuwainua kitaaluma wanasayansi vijana wa Tanzania zimeleta maajabu yakiwamo kugundua namna bora ya kufuga kwa tija, lakini kwa mbinu na gharama nafuu.

Jitihada hizo zinazowahusu wanafunzi wenye vipaji na ubunifu, wadau huwaibua na kuwapa hamasa na msaada wanaohitaji kuendeleza vipaji na ugunduzi huo wa kisayansi.

Young Scientists Tanzania (YST), ndiyo 'huwaatamia' wanafunzi wa sekondari kwa kuwashindanisha na kuwaandalia tuzo za kisayansi kila mwaka.

Licha ya safari hii kuwa na corona, kazi hiyo ilifanyika kwa kwa njia ya mtandao, anasema mwanzilishi wa YST Dk. Gozbert Kamugisha.

Anaeleza kuwa kabla ya janga la COVID-19, YST ilikuwa inaandaa maonyesho ya kazi za kitafiti zilizofanywa na wanafunzi wa sekondari kuonyesha utafiti wa sayansi na teknolojia walioufanya kwa usimamizi wa walimu wao.

Hata hivyo, mwaka huu, washiriki waliziwasilisha kwa wataalamu na majaji wanaosimamia mashindano hayo ambao walitangaza matokeo na washindi kwa mtandao, anasema Dk. Kamugisha.

Anaeleza kuwa washindi wa mwaka huu ni kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Nganza mkoani Mwanza na kuongeza kuwa mwaka huu ni mara ya 10 kwa YST kuandaa tuzo hizo.

Mpaka sasa tangu mashindano haya ya YST yalipoanza, wanafunzi 20 wamenufaika na mradi huu wa kuwainua kupitia sayansi, ambapo wote walioshinda wamepatiwa ufadhili wa masomo kwa ngazi ya chuo kikuu, anasema Dk. Kamugisha.

Baadhi yao tayari wamehitimu masomo yao ya chuo kikuu na wengine wanaendelea kusoma, huku wengine wakimalizia elimu ya sekondari ili waweze kufaidi ufadhili wa masomo ya juu.

Kwa mfano, wanafunzi walioshinda tuzo mwaka 2014 ambao ni Dharia Amour Ali and Salma Khalfan Omar, hawa wanasoma shahada ya udaktari.

Washindi wa mwaka 2015 Edwin Luguku na John Method, Edwin anasoma shahada ya udaktari na John Method anasoma ufamasia.

### KILICHOWAPA USHINDI

Glory Kiroche na Martha Machumu kutoka Sekondari ya Nganza, mkoani Mwanza ndiyo washindi ambao wamepata medali na udhamini wa masomo ya chuo kikuu kutoka Taasisi ya Karimjee Jivajee Foundation, baada ya kuibuka washindi mwaka huu.

Kwa mujibu wa Glory Kiroche, kilichowapa ushindi ni ugunduzi wa chakula cha samaki kinachoandaliwa kwa kuchanganya nafaka za ngano na maji kisha kuzirutubisha na mbolea ya wanyama.

Anasema matokeo yake chakula hicho kiliongeza uzalishaji wa samaki na ng'ombe kwa haraka shuleni kwao. Baada ya wanafunzi hao kuibuka kidedea walizawadiwa tuzo za medali na kikombe pamoja na pesa taslimu Sh. milioni 1.35.

Glory mmoja wa washindi hao wa jumla wa YST mwaka huu, anasema katika kufanikisha kazi hiyo ya kitafiti walitumia mbinu mbalimbali ikiwamo kutenga muda wa kutafuta na kuchanganya sampuli tofauti kisayansi kwa ajili ya kupata matokeo chanya ya kazi waliyokuwa wameilenga.

Mshindi huyo anasema Sekondari ya Nganza inafuga samaki na inajishughulisha na kilimo na kwamba walikuwa wanapata shida hasa namna ya kupata chakula bora kwa ajili ya samaki na wakati mwingine walitumia gharama kubwa kuwalisha.

Aidha, vyakula vingine walivyotumia kwa mifugo havikuwa na lishe bora hivyo kuhatarisha ustawi wa mifugo hiyo na hata kuathiri kuzaliana.

Glory anasema baada ya kugundua mbinu hiyo walipata chakula ambacho walikijaribu kwa samaki wanaofugwa shuleni kwao na baada ya siku kadhaa walianza kuona matunda.

### MABADILIKO

"Baada ya majaribio yale ya awali tuliona mambo yanaanza kuwa mazuri, samaki walianza kung`ara na kukua haraka," anasimulia Glory.

"Tulipata matumaini na kuongeza nguvu ya kutengeneza chakula kingi zaidi na kuacha kutumia vingine ambavyo havikuandaliwa kitaalamu." Anaeleza mshindi huyo na kwamba walikuwa wakikizalisha kwa takribani siku saba.

Baada ya kugundua kwamba kinafaa kwa samaki walikijaribu kwa ng'ombe.

"Kwa mfano chakula hiki tulipokijaribu kwa ng`ombe wa maziwa, kiliongeza kiwango cha maziwa. Kwa mfano kama ulikuwa unazalisha lita tano, utazalisha mara mbili. Na pia ilionekana kuongeza uzito kwa mifugo kuliko kutumia majani ya kawaida."

Anasema baada ya kufanikiwa katika ugunduzi huo gharama walizokuwa wakitumia kabla ziliondoka.

> "Baada ya majaribio yale ya awali tuliona mambo yanaanza kuwa mazuri, samaki walianza kung`ara na kukua haraka.

### CHANZO CHA UGUNDUZI

Glory anasema walipata wazo kwa sababu shule ilikuwa ikitumia gharama kubwa kununua chakula cha mifugo na hiyo ikawa sababu kuwasukuma kufanya utafiti wa kugundua teknolojia ili kusaidia kuzalisha samaki wengi zaidi.

Akizungumzia tuzo za mwaka huu ambazo zilifanyika kwa njia ya mtandao, Mwenyekiti wa Bodi ya YST, Profesa Yunus Mgaya, anasema kuwa tuzo hizo mwaka huu zilijumuisha miradi zaidi ya 6,000 kutoka maeneo mbalimbali ikiwamo sayansi, hesabu, baiolojia na ikolojia, sayansi ya kijamii na teknolojia. Mwanzilishi wa Tuzo hizo za YST, Dk. Gozbert Kamugisha, anasema ni mara ya 10 tuzo hizo kufanyika nchini na zinalenga kuhamasisha na kutoa wahitimu wenye uwezo na ubunifu kusaidia kubadilisha jamii zao kupitia uvumbuzi.

"Tunaamini kuwa uwekezaji katika elimu hautasaidia kuboresha njia ya ufundishaji na utafiti katika nyanja ya sayansi tu, lakini pia, kuhamasisha zaidi wanafunzi shuleni kupenda sayansi."

Tuzo hizo hulenga kugusa katika nyanja mbalimbali ambazo lengo lake ni kutatua matatizo yaliyopo katika jamii ikiwamo katika sayansi ya kemia, fizikia na hesabu, biolojia na mazingira, sayansi ya jamii na teknolojia. Pia hugusa katika utatuzi wa matatizo ya afya, kilimo, mawasiliano na usafirishaji, nishati, mazingira, elimu na mahusiano kijamii.

Aidha, anasema wanafunzi wanasayansi chipukizi wanaoibuka kidedea katika ugunduzi huzawadiwa pesa taslimu pamoja na medali.

Aidha, washindi wa jumla hupata udhamini wa masomo ya chuo kikuu unaofanywa na Taasisi ya Karimjee Jivanjee Foundation inayowawezesha kusoma masomo ya sayansi na teknolojia pia huiwakilisha Tanzania katika maonyesho ya kimataifa.

Aidha, Dk. Kamugisha anaishukuru taasisi hiyo ambayo ni mdhamini mkuu wa tuzo hizo.



Martha Machumu (kushoto), Glory Kiroche na Mkuu wa Sekondari ya Nganza, Mageni Msambo, wakifurahia kombe na tuzo walizoshinda baada ya kuibuka washindi. **PICHA: YST**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, KAHAMA

# Kahama yawa kipaumbele elimu na ulinzi wa wazee



Wajumbe wa Baraza la Wazee wilayani Kahama wakiwa kwenye moja vikao vya kazi. **PICHA: MARCO MADUHU**

SERA ya Wazee ya mwaka 2003 inamtambua mzee kuwa ni yule mwenye zaidi ya miaka 60, ambaye atakuwa amemaliza nguvu ya kufanya kazi na anahitaji kupumzika.

Lakini licha ya sera kusema hayo kwenye baadhi ya jamii wazee wamepewa kisogo, na huonekana kama mikosi katika familia zao na kufikia hatua ya kuwafanyia ukatili ukiwamo kuwatelekeza, kuwanyanyapaa, kuwanyima chakula, pamoja na wengine kuuliwa wakiwatuhumiwa kuwa ni washirikina.

Mwaka 2018 Tanzania iliandaa mkakati wa kitaifa wa miaka mitano utakaomalizika 2023 uliolenga kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wazee. Shirika la TAWLAE linalotetea haki za wazee mkoani Shinyanga, limekuwa likishirikiana na serikali na wadau kupambana ili kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wazee ndani ya jamii. Likilenga kufanikisha azma hiyo ya serikali ya kumaliza matukio hayo ifikapo mwaka huo 2023.

Mratibu wa TAWLAE Eliasenya Nnko, anasema kutokana na kuendelea kuwapo na matukio ya ukatili dhidi ya wazee ndani ya jamii, akiitaja Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, kuwa kumekuwapo na matukio mengi ya ukatili dhidi ya wazee.

Anasema mkakati umezinduliwa ukifanyakazi ndani ya mwaka mmoja ukitarajiwa kumalizika Mei 2021.

Nnko anasema utekelezaji wa mradi huo unaanzia katika Wilaya ya Kahama kwenye matukio mengi ya ukatili dhidi ya wazee, ili kupunguza mauaji hayo ama kuyamaliza, baada ya hapo wataelekeza nguvu kwenye wilaya nyingine.

> “Matukio ya mauaji ya wazee wilayani hapa tumeyapunguza mwaka 2012 kulikuwa na mauaji 27, 2013 yaliripotiwa 21, wakati 2014 yalishuka hadi 15 na mwaka 2015 visa vilikuwa 19.

“Kitu ambacho tutakuwa tukifanya kwenye utekelezaji wa mradi wetu huu, ni kutafuta ufumbuzi wa tatizo, na kutokomeza matukio haya ya ukatili dhidi ya wazee, kwa kutoa elimu kwa wananchi kuwathamini wazee, kuwatunza, kutowatelekezea wajukuu, pamoja na kuacha mauaji dhidi yao kwa imani potofu za kishirikina,”anasema Nnko.

“Lengo la mradi huu unaofanywa kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia na Kujali Wazee la Helpage ni kuhakikisha ifikapo 2023 kama dira ya taifa inavyosema, kusiwapo na matukio ya ukatili dhidi ya wazee hapa nchini, bali tutizamie kwenye shughuli nyingine za kimaendeleo, na kuacha kuumiza vichwa kujadili utetezi wa haki za wazee tena,” anaongeza.

Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Kahama Mji, Jonathan Shayo, anasema matukio ya ukatili dhidi ya wazee yapo na serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inajitahidi kuyamaliza lakini hali siyo ya kuridhisha.

Anasema mwaka jana pamoja hadi Februari mwaka huu waliwarudisha wazee nyumbani kwao hasa waliokuwa wakiomba omba kwenye stendi ya mabasi wilayani humo na wengine waliokuwa wakilala kwenye maeneo ambayo si salama kiulinzi na hata kiafya.

Anafafanua kuwa, baada ya kuwarudisha wazee hao cha ajabu wamerudi tena kwenye kituo cha mabasi na kuendelea kuombaomba, na kuishi maisha ya tabu licha ya watoto wao kujiweza.

“Tatizo la wazee kuendelea kuishi maisha magumu tena kwenye mazingira hatarishi, linatokona na watoto au ndugu kuwafanyia ukatili wanapokuwa wakiishi nao, na kuwaona kama mikosi. Wengine wakiwatuhumu kuwa ni washirikina,” anasema Shayo.

“Baada ya wazee hawa kurudi na kuendelea kuwa omba omba, ilibidi nifanye uchunguzi na kugundua kuwa wamefukuzwa na watoto wao wakiwatuhumu kuwa ni washirikina, tena huyo mmoja watoto wake ni mafundi, lakini hawamtaki mama yao wakidai ni mchawi.”

“Serikali inachokifanya kwa sasa tumeandaa utaratibu wa kumpeleka mzee huyu kwenye kambi ya kulea wazee ya Kolandoto huko Shinyanga, ili akaishi sehemu salama, sababu tukilazimisha kwenda kuishi na watoto wake na tayari wameshamtuhumu kuwa ni mchawi wataweza kumuua,” amefafanua zaidi.

### KUWANYANYAPAA WAZEE

Monica Cosmas ni mzee ambaye anaishi wilayani Kahama, anasema matukio ya ukatili dhidi yao ni mengi, licha ya kupungua kwa mauaji ya vikongwe, lakini kuna matukio mengine bado yanaendelea, ikiwamo wazee kunyimwa chakula, mavazi, kuogeshwa, kulala sehemu chafu, pamoja na huduma za kiafya.

Anasema tatizo linalosababisha matukio hayo yote ni jamii kukosa elimu ya kuthamini wazee, na kuwaona hawana thamani tena na wakati wamewezaa, huku wakiendelea kuwatuhumu kuwa ni washirikina hasa wale ambao wana macho mekundu. Katibu wa Baraza la Wazee Wilaya ya Kahama, Underson Lyimo, anasema kwa sasa baraza hilo kwa kushirikiana na TAWLAE, serikali, polisi na wadau wengine wapo kwenye utekelezaji wa mradi ambao utakuwa mwarobaini wa kupunguza ama kutokomeza kabisa matukio ya ukatili dhidi ya wazee.

Anasema baada ya kutolewa elimu ya kutosha kwa wananchi kuwathamini wazee na kuacha kuwafanyia ukatili, kitakachofuata baada ya hapo ni kukamatwa na kuchukuliwa hatua, sababu masuala ya ukatili ni kosa kisheria na ukiukwaji wa haki za binadamu.

### MUHALI NI TATIZO

Elias Sikanda ni Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi wilayani Kahama, anasema matukio ya ukatili dhidi ya wazee wilayani humo ni mengi, ambapo mengine yamekuwa hayatolewi taarifa na kushindwa namna ya kuchukua hatua.

Anasema wazee ambao wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya ukatili, wengi wanaogopa kutoa taarifa kwa madai ya kuona uchungu endapo mtoto wake akikamatwa, na hivyo kuamua kutoshtaki na kuondoka nyumbani kuwa ombaomba mitaani.

Hali hiyo ya kuoneana aibu au muhali imewasababishia kurejea tena mitaani.

Aidha, anasema kazi ya Jeshi la Polisi ni kufanyia kazi mashtaka, na kama hakuna mashtaka haliwezi kuchukua hatua, na hivyo kuwaomba wazee ambao wanafanyiwa vitendo vya ukatili, washirikiane na baraza la wazee ili wasaidie kufungua mashitaka na kisha watuhumiwa wachukuliwe hatua.

“Ili ufumbuzi wa tatizo hili liweze kupatikana la kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wazee.

Anasema licha ya elimu kutolewa, pia taarifa zifikishwe polisi dhidi ya watu ambao wanafanya ukatili kwa wazee na kwamba wakipatikana hata wachache hatua zitachukuliwa na kushikishwa adabu hakutakuwa tena na matukio haya, kwa mujibu wa Sikanda.

“Matukio ya mauaji ya wazee wilayani hapa tumeyapunguza mwaka 2012 kulikuwa na mauaji 27, 2013 yaliripotiwa 21, wakati 2014 yalishuka hadi 15 na mwaka 2015 visa vilikuwa 19.

Mwaka 2016 yalikuwa manne, 2017 waliuawa wawili wakati 2018 yaliripotiwa mauaji ya wazee watatu huku 2019 na 2020 mpaka sasa hakuna kifo cha mzee kitokanacho na imani potofu za kishirikina,” ameongeza.

Sikanda anawataka pia viongozi wa kidini, nao waingie vitani kutoa elimu kwa jamii juu ya kupinga matukio hayo ya ukatili dhidi ya wazee, pamoja na kuwa na hofu ya Mungu ikiwa bila ya wao kuwa zaa wasinge kuwapo hapa duniani, bali wawatunze kama jinsi wao walivyo watunza wakiwa bado wadogo hadi wamekuwa watu wazima.

# EAGT yamchagua Mwakipesile Askofu Mkuu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KANISA la Evangelistic Assemblies of God Tanzania (EAGT), limemchagua Dk. Brown Mwakipesile, kuwa Askofu Mkuu wa kanisa hilo kuongoza tena kwa kipindi cha miaka mitano.

Akizungumza juzi baada ya kuchaguliwa kwenye mkutano wa taifa uliohudhuriwa na wachungaji na wainjilisti, Askofu Mwakipesile alishukuru kanisa hilo kwa kumwamini tena kuongoza.

"Nimetupiwa madongo mengi kumbe Mungu bado ananihitaji kufanya kazi yake namshukuru hayati Moses Kolola kwa kuacha misingi imara na EAGT haitatetereka kazi ya Mungu itasonga mbele," alisema.

"Mkutano huu ulipita ilikuja barua kutoka mahakama ikisema wadhamini wafutwe ilimradi tu kanisa lisambaratike, lakini Mungu ni Mkuu tulishinda kesi na uchaguzi ukafanyika siku zote kazi ya Mungu itasonga ukishtaki kanisa ni sawa umeshtaki Yesu."

Akifungua mkutano huo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, aliwaomba viongozi wa dini kuombea nchi uchaguzi mkuu ufanyike kwa amani na utulivu ili kupata viongozi bora.

Alimuomba Askofu Mwakipesile kuhimiza waumini kwenda kupiga kura Oktoba 28 ili kuchagua viongozi bora na kuifanya Tanzania kuendelea kuwa kisiwa cha amani.

Pia alisema viongozi hao wana kazi ya kusimamia maadili ya watu hasa vijana.

Kabla ya uchaguzi huo kufanyika, Katibu Mkuu wa EAGT Taifa Askofu Dk. Leonard Mwizarubi, alibainisha mafanikio yaliyopatikanani pamoja na kuwa na mpango mkakati wa miaka 15, kusajili Bodi ya Wadhamini na kuwekeza kwenye miradi mbalimbali.

# Mabadiliko tabia nchi yashusha uzalishaji zabibu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MABADILIKO ya tabia nchi yaliyochangia kuongezeka kwa mvua Mkoa wa Dodoma mwaka 2020 ni miongoni mwa sababu za kupungua kwa uzalishaji wa zabibu msimu huu.

Nipashe mwishoni mwa wiki ilitembelea maeneo maarufu na yenye mashamba makubwa ya zabibu katika kata ya Mpunguzi, Mbabala na Hombolo na kubaini kuwapo na uzalishaji mdogo ikilinganishwa na misimu iliyopita.

Wakizungumza hali hiyo, wakulima hao walisema kwa mwaka huu uzalishaji sio mzuri kwa kuwa zimeadimika kabla ya msimu kuisha.

"Mwaka huu mavuno yalikuwa kidogo kutokana na mvua kunyesha sana, yaani kwa kiwango kikubwa miche iliishia kupata maua bila kuzaa na mingine iligoma kabisa kutoa matunda," alisema mkulima Maneno Joseph.

Alisema mwaka huu kwao ni hasara kutokana mavuno kidogo licha ya kuwapo na bei nzuri kwenye soko.

"Unakuta shamba lilikuwa la kuvuna tani tano za zabibu, lakini amevuna kilo 600, au shamba lingine kama mkulima alichelewa kuliandaa basi hajapata kapiga," alisema.

Kadhalika, Nipashe ilizungumza na wachuuzi wa zabibu ambao nao walieleza kilio chao kuwa kwa sasa zabibu hazipatikani kwa urahisi na huweka oda siku mbili au tatu ndio wape mzigo tofauti na ilivyokuwa awali kila siku kupata mzigo.

Mmoja wa wachuuzi, Zawadi Manzije, alisema biashara imekuwa ngumu kwao kutokana kuuziwa kwa gharama kubwa.

"Wateja wanajua zabibu zinalimwa hapa na ni bei rahisi, hivyo akikuta anauziwa kichane kimoja kwa Sh.1,000 au 2,000 analalamika maana amezoea kununua ile ya Sh. 1,000 kwa Sh.300 hadi 500," alisema.

Kwa upande wake, mmiliki wa kiwanda cha kutengeneza mvinyo cha Alko Vintages, Archard Kato, alisema mahitaji ya zabibu yamekuwa makubwa licha ya wakulima kuongeza zaidi uzalishaji.

"Kutokana na hali hii wameathirika wakulima kutokana na mazao yao kupungua na hata sisi wasindikaji pia tumeathiriwa na hali hii," alisema.

Akizungumzia hali hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alikiri kuwa uzalishaji wa zabibu msimu huu umeshuka huku akitaja sababu kuu mbili kuwa ni mvua kubwa na kuyumba kwa soko la dunia kutokana na uwapo wa ugonjwa wa corona.

"Ni wazi kabisa katika maeneo mengi nchini mvua zilikuwa nyingi na zimefika kwenye maeneo ambayo zabibu inalimwa ikiwamo Mkoa wa Dodoma, sasa ilipotokea na ilisababisha baadhi ya mazao kuoza, zabibu ikifikia hatua ya kuiva na ikapata mvua kubwa mara nyingi zinaoza, uzalishaji tutarajie kushuka zaidi," alisema.


Alisema kwa msimu uliopita uzalishaji wa zao hilo uliongezeka na kufikia tani 15,000 ikilinganishwa na mwaka 2015/16 tani 8,336.

Alitaja mikakati ya wizara kuhakikisha uzalishaji unakuwa mkubwa ni pamoja na serikali kukijengea uwezo Kituo cha Utafiti cha Makutupora kwa ajili ya uzalishaji wa miche ya zabibu kinachotakiwa kuzalisha miche kutoka 100,000 hadi 300,000.

"Kituo kimepewa fedha na wizara na pia kimenunuliwa trekta jipya kwa ajili ya kutanua uzalishaji na kuwa na mashamba mengi ya miche ambayo itachukuliwa na wakulima," alisema.

Kadhalika, alisema wizara imeunda kikosi kazi cha wataalamu kufuatilia mwenendo wa zao hilo ili kutoa mapendekezo yao na kufanyiwa kazi.

"Wizara imeingia makubaliano na kampuni ya bia nchini TBL kutakuwa na vijiji 10 ambavyo vitaanzisha mashamba ya mfano na kufadhiliwa na kampuni hiyo, na tuna hakika kila kijiji kitakuwa na wakulima watatu, tuna imani itakuwa ni nafasi nzuri kwa wakulima kujifunza," alisema.



Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya (kushoto), akizungumza na wajumbe wa Baraza la Ujuzi wa Kilimo nchini (TPSF-ASSC), jijini Dodoma jana, baada ya kupokea mpango mkakati wa baraza hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**.

# Serikali kufanya kampeni kuhamasisha utunzaji wazee

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema katika maadhimisho ya Siku ya Wazee mwaka huu, kutakuwa na kampeni maalum ya kuhamasisha uundwaji wa mabaraza na jamii kuwajibika kuwatunza wazee.

Hata hivyo, Oktoba mosi mwaka huu hakutakuwa na maadhimisho ya kitaifa badala yake yatakuwa yakifanyika kila baada ya miaka miwili huku mikoa na halmashauri ikifanya kila mwaka.

Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii anayeshughulikia huduma za ustawi na maendeleo kwa wazee, kwenye Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, Mwanaisha Moyo aliyasema hayo mwisho mwa wiki katika kikao cha kutathmini mradi wa uwajibikaji kwa wazee Tanzania.

Mradi huo wa miaka miwili kuanzia mwaka 2018-2020, unasimamiwa na AcT-KPMG(Programu ya uwajibikaji Tanzania), kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID) na unatekelezwa na Shirika lisilo la serikali la Helpage International kwenye mikoa 10 ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Moyo alisema uundaji wa mabaraza ya wazee yatahamasishwa kwa kiwango kikubwa kwenye maadhimisho hayo.

"Kikubwa zaidi ni kuhamasisha jamii na familia kushiriki katika kuwatunza wazee," alisema.

Akizungumzia maadhimisho hayo, Kamishna Moyo alisema, awali walikuwa wakiadhimisha kitaifa kila mwaka sasa, lakini wamekaa na kufanya tathmini na wazee na kubaini maazimio mengi yanakuwa hayajapata muda wa kutosha kufanyiwa kazi.

"Tumeona mwaka ni mdogo tunaweka maazimio mengi, tujikuta mwaka unafika hatujafikia tukajipa tufanye kila baada ya miaka miwili, lengo ni mafanikio yanayopatikana yapate muda wa kutosha na yawe wazi," alisema.

"Kila mwaka tutakuwa tunaendelea na maadhimisho ngazi za mikoa na halmashauri, wizara tutashiriki katika mkoa mmoja wapo na kwa mwaka huu tutashiriki Mkoa wa Dodoma ambao umepanga kufanya maadhimisho kwenye Halmashauri ya Mji wa Kondoa."







Mgombea ubunge Jimbo la Mbeya Mjini kwa tiketi ya CCM, Dk. Tulia Ackson (aliyevaa kofia nyeusi), akishiriki shughuli za usafi wa mazingira kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya juzi, ikiwa ni jitihada za utunzaji mazingira. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Viongozi wa dini waonywa kuhubiri siasa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewaonya viongozi wa dini kutohubiri siasa kwenye nyumba za ibada badala yake wajikite katika kuhubiri injili na amani ya nchi.

Chalamila alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na Nipashe, ambapo alisema baadhi ya viongozi wa dini wamekuwa sehemu ya kuhubiri masuala ya kisiasa huku wakiwahamasisha waumini kuchagua chama fulani, huku wakitumia lugha ya Kiingereza katika maubiri yao.

Chalamila aliwaonya viongozi hao na kwamba huenda wanafanya hivyo kwa mashinikizo ya watu fulani tena kwa kutumia lugha ya Kiingereza ili watimize malengo yao.

"Nawaomba viongozi ambao wanatumiwa kuhubiri masuala ya siasa kwenye madhabahu kuacha mara moja kwani kwa kufanya hivyo kunaweza kuhatarisha amani ya nchi hasa kwa mkoa wangu wa Mbeya, sitakubali kuona masuala hayo yanafanyika," alionya Chalamila.

Chalamila aliwaomba wakazi wa Mbeya kutokubali kurubuniwa na maneno ya baadhi ya viongozi wa dini pamoja na wanasiasa ambao wanachochea uvunjifu wa amani.

Vile vile, aliwaomba wananchi kujiandaa kikamilifu kumpokea Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi ambaye ni Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kuja kuomba kura za kutosha zitakazomsaidia kuwa Rais.

Alisema mwenyekiti huyo amefanya mambo makubwa na mazuri katika kuboresha na kujenga miradi mbalimbali ya maendeleo katika ujenzi wa shule, barabara na hospitali.

Mgombea ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk, Tulia Ackon, alisema ujio wa Mwenyekiti wa Chama hicho utaleta matumaini kwa sababu ataahidi masuala mbalimbali ya maendeleo, hivyo wananchi wanapaswa kujitokeza kwa wingi kumsikiliza Septemba 30, atakapohutubia

# Serikali yaombwa mafunzo kukabiliana na uhalifu majini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KATIBU Mkuu wa Chama cha Mabaharia nchini, Kapteni Josiah Mwakibuja, ameshauri serikali kutoa mafunzo maalum ya kuogelea kwa askari wa Idara ya Uhamiaji ili waweze kukabiliana na vitendo vya uhalifu majini.

Kapteni Mwakibuja alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki wakati wa kilele cha maadhimisho ya siku ya usafiri kwa njia ya maji duniani ambayo kitaifa yalifanyika katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya.

Alisema ili kuongeza ufanisi na udhibiti wa vitendo vya uhalifu wakati wa kufanya doria ni lazima askari hao wakajifunza kuogelea iwe kuwakabili wanaopita kwenye njia za panya.

"Katika maadhimisho haya lazima askari wa uhamiaji ambao mara nyingi wanafanya doria za ulinzi wa mipakani wanapaswa kupata mafunzo maalum ya kuogelea sio kwamba hawajui, lakini wanapaswa kupatiwa mbinu nyingine ambazo zitasaidia kukabiliana na maadui ambao wanaopita kwenye njia za panya kwa kutumia maji," alisema Mwakibuja.

Aidha, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema kupitia maadhimisho hayo wananchi walipata nafasi ya kujifunza mbinu mbalimbali za uokozi na kuogelea ndani ya Ziwa Nyasa ili iwe rahisi kuokoa maisha ya watu wanaopata tatizo ndani ya maji.

Maadhimisho hayo ambayo yalishirikisha vikosi mbalimbali ya usafirishaji majini kutoka Tanzania Bara na Visiwani yalieleza mambo mbalimbali wanayoyafanya katika kuboresha sekta ya usafiri wa maji.

Chalamila aliwashauri wananchi wa Kyela kutumia vyema fursa ya uwapo wa Bandari ya Itunge na ujenzi wa meli tatu ambazo ni za mizigo na abiria kuhamasisha watoto wao kusoma masomo yanayohusu sekta ya maji ikiwamo ubaharia ili kupata ajira kwa urahisi.

Aliongeza kuwa uwapo wa meli hizo utapunguza gharama kubwa ya ununuzi wa bidhaa ikiwamo saruji ambapo kupitia Ziwa Nyasa zitasafirishwa na kuuzwa kwa bei nafuu.

Kwa upande wao Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) Kamandi ya Kanamaji, walisema kuwa moja ya majukumu yao ni kutoa elimu kwa wananchi juu ya shughuli za uokoaji pindi yanapotokea majanga.

Mmoja wa askari hao, Francis Mkondya, alisema mafunzo waliyoyapata sio tu yaweza kukabiliana na adui wawapo majini, lakini wanalojukumu la kufanya uokoaji katika maeneo mbalimbali yanayotokea maafa.

Alisema moja ya kazi waliyowahi kufanya ni uokoaji wa ajali ya maji iliyotokea katika kisiwa cha Ukerewe, ambayo iliua Watanzania wenzetu.

Mkurugenzi wa Utawala na Utumishi, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Sekta ya Uchukuzi, Lucas Kambelenje, alisema siku ya usafiri kwa njia ya maji duniani, inatoa nafasi kwa sekta hiyo kusikiliza kero za wananchi zinazoikabili sekta hiyo na kuzitatua.

Alisema usalama wa abiria na chombo cha usafiri wa maji kinategemea ujuzi na utaalamu sio tu kwa wataalamu, bali na ushirikiano na wananchi, hivyo elimu ya ukoaji itasaidia kukabiliana na vikwazo mbalimbali vya majini.

# Wajasiriamali wilaya Chunya wakopeshwa milioni 155/-

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

JUMLA ya shilingi milioni 155 zimetolewa kwa vikundi 18 vya ujasiriamali vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya ikiwa ni lengo la serikali kuwakwamua wananchi kiuchumi.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, ndiye alikabidhi kiasi hicho cha fedha jana kwa vikundi 18 vya wajasiriamali ikiwa ni utekelezaji agizo la serikali kutenga asilimia kumi ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mayeka alisema miongoni mwa wanufaika ni kundi la wanawake, vijana na wenye ulemavu, na kwamba moja ya masharti wanayotakiwa kuzingatia ni kuhakikisha mikopo hiyo inarejeshwa kwa wakati ili na wengine waweze kukopeshwa.

Alisisitiza kuwa halmashauri haitasita kuchukua hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani kwa watakaokaidi kulipa mikopo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani humo, James Sunge, alisema kwa kipindi cha Januari hadi Juni mwaka huu, kiasi cha shilingi milioni 600 zimekopeshwa kwa vikundi mbalimbali vya wajasiriamali ambavyo tayari vilijisajili na kuwa na sifa ya kukopesheka na marejesho ya fedha hizo yanaenda vizuri.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya hiyo, Sophia Kumbuli, alisema utaratibu wa utoaji mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali ili kuwawezesha kufanya shughuli zao na kujikwamua na umaskini ni agizo la serikali, na kwamba wanaendelea kutafuta vyanzo vingine vya mapato kupitia mapato ya ndani ili kuwafikia watu wengi zaidi.

"Wanawake wengi sasa wanamiliki pesa na viwanda mbalimbali vya kuzalisha bidhaa, hali ambayo imesaidia kupunguza migogoro na vipigo ndani ya ndoa kwa sababu wanajitegemea," alisema Kumbuli.

Baadhi ya vikundi vilivyonufaika ni cha vijana Sabasaba ambapo Omary Mashauri ni miongoni mwa wanufaika, alisema kupitia mkopo wa shilingi milioni tano, uliwasaidia kufungua mradi wa kufungua mradi wa kiwanda cha kufyatua matofali.

Mwenyekiti wa kikundi cha kusindika mafuta ya alizeti, Ngailo Thobias, alisema walipewa mkopo wa Sh. milioni 14 ambazo walizitumia kuanzisha kiwanda na kutoa ajira, huku Evarist Fusi akisema kupitia mikopo hiyo wamesaidia kuongeza ajira kupitia uanzishwaji wa vikundi.

Wengine Beatrice Kalinga na Theresia Kayombo walisema wanawake wamenufaika na mikopo kwani hivi sasa wamefungua kiwanda cha kuchakata nafaka na kutengeneza batiki na wanasomesha watoto kupitia faida.

# Wasaidizi kisheria muhimu kwa jamii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Msaada wa Kisheria Zanzibar, Hanifa Ramadhan Said, amesema wasaidizi wa sheria wana umuhimu mkubwa katika jamii kutokana na kazi zao za msaada wa kisheria.

Aliyasema hayo katika mkutano wa pili wa robo mwaka wa kuratibu masuala ya msaada wa kisheria uliofanyika ukumbi wa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale Kikwajuni, mjini hapa.

Alisema jitihada hizo wanazozifanya wasaidizi wa sheria zinahitaji kutambuliwa na kuthaminiwa ili kuwapa hamasa ya kuendeleza kufanya vizuri.

Alisema kuwa sheria ya msaada wa sheria imewatambua wasaidizi hao kama ni watoa msaada hivyo wanahitajika kufanya kazi zao kwa mujibu na taratibu.

"Sera ya msaada wa kisheria ya mwaka 2017 katika hoja ya tatu inayojulikana upatikanaji mdogo wa huduma za msaada wa kisheria na watu maskini na wenye mahitaji maalum...ambapo katika hoja hii moja ya mkakati wake wa pili ni kuimarisha mafunzo, utoaji vyeti, utambuzi na motisha kwa wasaidizi wa sheria," alisema Mkurugenzi huyo.

Akisoma ripoti ya mwaka ya utekelezaji wa shughuli za idara ya msaada wa kisheria, ofisa sheria, Salma Suleiman alisema idara hiyo imewafikia wananchi 338 wa shehia nne za Unguja kwa kuwapa elimu ya kanuni na sheria za msaada wa kisheria na kwa Pemba wamewafikia wananchi 150 katika Wilaya ya Micheweni.

Alisema Idara pia imekamilisha kutayarisha mfumo wa usajili kwa njia ya kielektroniki kwa ajili ya kuwasajili watoaji wa huduma wa kisheria.

Alisema mfumo huo kwa sasa unapelekea utambuzi wa watoaji msaada wa kisheria na kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi za watoa huduma za msaada wa kisheria pamoja na wataka huduma hizo.

Kadhalika alisema kwa kipindi cha mwaka idara inajivunia mafanikio mbalimbali ikiwamo kusimamia vizuri jukumu la kuratibu shughuli za msaada wa kisheria, kujenga ushirikiano wa karibu kati ya watoa huduma za msaada huo na wadau wengine na kukamilisha mwongozo wa usajili wa watoa msaada wa kisheria.

"Kwa upande wa changamoto inayoikabili idara ni kuanzishwa kwa idara hiyo wakati bajeti ya serikali imeshapitishwa hivyo kuleta changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa baadhi ya shughuli," alisema.

Kwa upande wao washiriki walisema kuwa wasaidizi wa sheria wanafanya kazi kubwa katika jamii, lakini baadhi ya watu hawatoi ushirikiano hali inayowafanya kufanya kazi katika mazingira magumu.



Mkurugenzi wa Idara ya Msaada wa Kisheria ya Wizara ya Katiba na Sheria Zanzibar, Hanifa Ramadhan Salum (kushoto), akizungumza katika kikao cha uwasilishaji wa ripoti kuhusu wasaidizi wa huduma za kisheria, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mke mgombea awataka watoto kike kujitambua

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Maryam Mwinyi, amewataka watoto wa kike kujitambua kwa kufuata mila silka na tamaduni zao na kujenga heshima na tabia njema ili kuwa watoto wa mfano kwa Zanzibar.

Alisema mtoto wa kike ni nguzo muhimu katika jamii na maendeleo kwa ujumla.

Akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Mwanawake Benbella Mjini Zanzibar, alisema watoto wa kike wamekuwa wakiiga tamaduni za nje kupitia mitandao ya kijamii na kupoteza mwelekeo wa ndoto zao katika maisha ya baadaye.

"Nawasihi sana wanangu mjitambue kuwa watoto wema msiige tamaduni za kigeni sio mila zetu, tufateni misingi ya dini yetu kwa kutengeneza jamii iliyobora," aliwaasa.

Alisema, watoto wa kike wanapaswa kutambua kuwa ni mama watarajiwa katika sekta mbalimbali nchini na hata katika familia zao.

Hata hivyo, alisema elimu ni ufunguo wa maisha na msingi mkuu wa maendeleo hivyo ni vyema kujikita katika kusoma na kuacha kudanganywa na watu ambao wanataka kuwakatisha ndoto zao.

"Msikubali kudanganyika kuweni na ndoto na matarajio katika maisha yenu ya baadaye taifa linahitaji viongozi mkiwamo nyinyi vitu vingine vipo jielekezeni kwenye masomo huo ndio wajibu wenu kwa sasa kwa kuwa mshika mbili moja humponza," aliwasisitiza.

Aliwataka wanafunzi kupenda masomo ya sayansi kwa kuwa dunia ya sasa inakwenda kwa sayansi, teknolojia na dijitali.

Hata hivyo, aliwashauri kuwa raia wema katika kuipenda nchi yao na kuwa walinzi wa amani ili kuleta maendeleo.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, alisema lengo la serikali kuanzisha madarasa maalum ya wanawake ni ufaulu na idadi kubwa ya wanawake ikilinganishwa na wanaume.

Alisema serikali inajitahidi kufanya mambo mengi katika sekta ya elimu, lakini changamoto za kila siku zinakuwapo kutokana na kuongezeka kwa wanafunzi mwaka hadi mwaka hasa watoto wa kike kuwa na mwamko wa kusoma.

Kwa upande wake Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Zainab Mbwana Mgunda, aliipongeza serikali ya awamu ya saba chini ya Rais wa Zanzibar katika kutatua changamoto mbalimbali katika shule hiyo ikiwamo madawati.

Alisema idadi ya wanafunzi imekuwa ikiongezeka siku hadi siku kutokana na serikali kuweka misingi mizuri ya upatikanaji wa elimu nchini.

Wanafunzi wa shule hiyo walisema wanakabiliwa na changamoto mbalimbali hasa upungufu wa vitabu na madarasa hasa kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita ambayo inashusha ufaulu wao kutokana na kutosoma kwa wakati.

# Z'bar yajivunia miradi ya uchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi amesema Zanzibar inajivunia kasi kubwa iliyopiga ya miradi ya kiuchumi na maendeleo ndani ya kipindi kifupi kutokana na usaidizi uandamizi mkubwa unaoendelea kufanywa na taifa rafiki la Jamhuri ya Watu wa China.

Alisema ipo miradi ya wazi inayoshuhudiwa na wananchi na Jumuiya za kimataifa ambayo tayari inaendelea kuwafaidisha watu wakati mingine ikiwa katika hatua za mwisho kukamilika ikilenga kustawisha maisha ya jamii na kuongeza pato la taifa.

Balozi Iddi alisema hayo wakati akizungumza na Balozi mdogo wa Jamhuri ya Watu wa China, aliyepo Zanzibar Xie Xiuow, aliyefika ofisini kwake Vuga, kuaga baada ya kumaliza muda wake wa miaka minne ya utumishi wa kidiplomasia visiwani humo.

Alisema Jamhuri ya Watu wa China imekuwa mshirika wa karibu na Zanzibar na Tanzania kwa ujumla baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 na imekuwa ikiunga mkono miradi ya maendeleo katika taasisi mbalimbali za umma na binafsi.

Balozi Iddi alisema miradi iliyoanzishwa kwa ushirikiano kati ya pande hizo mbili kama ujenzi wa kiwanda cha sukari, Mahonda, viwanda vya sigara na viatu Maruhubi, mashamba ya kilimo Upenja na Bambi sekta zilizotoa mchango mkubwa wa kitaalamu na ajira kwa wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba.

Vile vile, alimpongeza na kumshukuru Balozi huyo kwa usimamizi wake mkubwa wa ushirikiano wa kidiplomasia uliosababisha kuibuka kwa miradi mingi ya kiuchumi na maendeleo ndani ya kipindi chake cha miaka minne Zanzibar.

Balozi Iddi aliitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni pamoja na uimarishaji wa miundombinu ya sekta ya maji, ujenzi wa shule za sekondari, huduma za afya hasa kipindi cha mpito wakati wa mlipuko wa virusi vya corona.

Alisema China licha ya kuwa na idadi kubwa ya watu wanaokadiriwa kufikia zaidi ya bilioni 1.4 wanaohitaji huduma za msingi katika ustawi wao, lakini bado imezingatia kuendelea kuiunga mkono Zanzibar kuona wananchi wa visiwa hivyo pia wanaendelea kudumisha ustawi wao.

Naye Balozi mdogo wa China Xie Xiuow, alisema anajisikia faraja kuona kwamba miradi mikubwa iliyoanzishwa ndani ya kipindi chake cha miaka minne iliyopata msukumo kutoka Jamhuri ya Watu wa China imekamilika na mingine ikiwa katika hatua za mwisho.

Alitolea mfano ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Abdullah Mzee iliyopo mkoani Pemba, upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar, viwanja vya michezo vya Mao Tse Tung, jengo la shule iliyopo Mtaa wa Mombasa, uwekaji wa taa za barabarani katika maeneo ya miji pamoja na usimamizi wa mafunzo ya juu kwa wanafunzi wa visiwa hivyo nchini China.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**BEACH PLOT FOR SALE**

PLOT SIZE: - 0.91 Acres (3682.64 Square Meters)
LOCATION: - PLOT NO 40, KUNDUCHI BEACH, NEXT TO SILVER SANDS,DARESALAAM CITY
DESCRIPTION: - DIRECT ACCESS TO THE BEACH.
INTRESTED BUYERS MAY CONTACT +255 753786114

## VIWANJA/MASHAMBA

**Eneo linapangishwa/kuuzwa**

Eneo linapangishwa/ kuuzwa ukubwa wa mita mraba (sqm) 3,130, Tabata Liwiti, Dar es Salaam. Liko katika barabara kuu na inafaaa kwa ajili ya kujenga kituo cha mafuta, super market nk. Wasiliana kwa simu: 0715624747/0767235965.

## VIWANJA/MASHAMBA

**PRIME PLOT FOR SALE**

PLOT SIZE: - 14.87 HECTARE (36.74 ACRE)
LOCATION: - BAGAMOYO DISTRICT, BLOCK C SANZALE, LOCATED ON MAIN ROAD, 5 MIN FROM BAGAMOYO TOWN,3 KM AWAY FROM ROUND ABOUT
DESCRIPTION: - THE PLOT IS FURTHER DIVIDED IN 5 DIFFERENT TITLES.
INTRESTED BUYERS MAY CONTACT +255 753786114


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


**MAHAKAMA YA ARDHI NYUMBA YA WILAYA MBEYA**
**MAOMBI NO. 283/2018**

**GIDA MAIDI ..............................**
**..........................................MLETA MAOMBI**

**DHIIDI YA**
**BUHOLO MANDALU**
**..................................................MJIBU MAOMBI**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA: BUHOLO MANDALU**

Fahamu kwamba maombi yamefunguliwa dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 27/10/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh. A. Mapunda Mwenyekiti wa baraza. Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria. Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya Mjiini.
Kumbuka: usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri / Muhuri wa baraza hili leo tarehe 24/09/2020

## KUPOTEA KWA KADI

Jesse Jackson Muheta anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA BREVIS usajili namba T434 DEL, Iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: DAR/MSI/RB/681603/2020

**MWAMBA MILLENIUM COMPANY LIMITED**
**CHIMWAGA DODOMA**
**Plot No.4 BLOCK Na.13**
**P.O.BOX 3221**
**Tel No: 0767245977/0717073423.**
**Email:Mwamba@yahoo**
**TANGAZO TANGAZO TANGAZO**
**TAREHE 21/09/2020**
**SHAURI LA MADAI NAMBA:250/2018**
**KWA AMRI YA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA MJINI**
**MNADA WA HADHARA**

TUTAENDESHA MNADA WA HADHARA WA KUUZA NYUMBA ILIYOPO MAHUNGU KIWANJA NAMBA 129 KITALU 'H' MAHUNGU JIJINI DODOMA MALI YA BWANA DONALT MAULID MAKUTU NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14) ILI KUFIDIA DENI ANALODAIWA NA BWANA ISAAC JOSEPHAT MWAIPOPO, MNADA UTAFANYIKA TAREHE 05/10/2020 SAA NNE ASUBUHI(10:00AM).
MASHARTI YA MNADA: -

- UKAGUZI UNARUHUSIWA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.
- MALIPO 25% BEI ITAYOWEKWA KWENYE MNADA
- ENDAPO MNUNUZI ATASHINDWA KULIPA SALIO KWA MUDA ULIOWEKWA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI ZOTE
- KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA KWA SIMU NAMBA 0712245977, 0754303498 AU 0719292430.

NATHAN J KAUNDA
MKURUGENZI MTENDAJI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

TIMOTHEO BARNABAS RUBI ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 499 AWS. YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: MTW/MTW/RB/617076 /2020.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;285/2020**

Ombi la VUMILIA HAMIDU SANGARI,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HAMIDU MZEE SANGARI.Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 01/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 22/09/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU

## KUPOTEA KWA CHETI



**WILSON JAPHET NGEMELO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0127/0059 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ST. PIUS X MAKOKO SEMINARY mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No: 9910819238115.


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi
Kwa Bei Poa Tupigie
0782253676

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Waziri akatwa mshahara kutumia ndege ya kijeshi

**JOHANESNBURG,** Afrika Kusini

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, amemkata mshahara Waziri wa Ulinzi kwa miezi mitatu, baada ya kuruhusu maofisa wa chama tawala kusafiri kwa kutumia ndege ya jeshi hadi nchini Zimbabwe pamoja naye, Septemba 9.

Nosiviwe Mapisa-Nqakula, alishutumiwa kwa kuruhusu matumizi ya rasilimali ya taifa kwa sababu za siasa za chama.

Jeshi la nchi hiyo lilikuwa limeeleza kwamba, waziri huyo alikuwa katika ziara rasmi ya kitaifa na kwamba aliwafanyia abiria wengine hisani kwa kuwabeba.

Rais Ramaphosa, aliitaja hatua hiyo kama makosa.

**Wasasiasa wa upinzani walimkosoa vikali waziri huyo kwa sababu aliandamana na ujumbe wa Chama cha ANC.**

Mapisa-Nqakula alienda mji mkuu wa Zimbabwe, Harare, kuhudhuria mkutano uliokuwa umepangiwa kujadili masuala ya kanda.

Ujumbe kutoka chama tawala cha Afrika Kusini - African National Congress (ANC) - ulikuwa unahudhuria mkutano huo kwa mazungumzo ya dharura na chama tawala cha Zimbabwe Zanu-PF lengo lao, likiwa ni kutatua mgogoro wa kisiasa na kiuchumi nchini humo.

Lakini, wasasiasa wa upinzani walimkosoa vikali waziri huyo kwa sababu aliandamana na ujumbe wa Chama cha ANC.

Raos Ramaphosa, ambaye kipindi anaingia madarakani aliahidi kumaliza sifa mbaya ya Chama cha ANC baada ya mwongo mmoja wa kashfa za ufisadi, alisema kwamba “kwa kuandamana na wajumbe wa ANC kwa ndege aliokuwa anatumia, hakufanya uamuzi stahiki unaozingatia uongozi mzuri”.

Alisema ameamua kumkata mshahara Mapisa-Nqakula na pesa hizo zitaelekezwa mfuko wa kusaidia kukabiliana na janga la corona.

**Wakati huo huo,** Chama cha upinzani cha Democratic Alliance kilisema, hatua iliyochukuliwa na bwana Ramaphosa haitoshi.

Suala hilo huenda likajadiliwa zaidi bungeni huku kukiwa na wito wa waziri huyo kufutwa kazi. **BBC**



Mapisa-Nqakula, Waziri wa Ulinzi wa Afrika Kusini, amekatwa mshahara na fedha hizo, zitaelekezwa katika mfuko wa kukabiliana na virusi vya corona, baada ya kuruhusu maofisa wa chama tawala kusafiri kwa kutumia ndege ya jeshi hadi Zimbabwe. **PICHA: BBC**

## Mali yapata waziri mkuu mpya

**BAMAKO,** Mali

RAIS wa mpito wa Mali, Bah Ndaw, amemteua waziri mkuu mpya.

Ndaw amemteua mwanadiplomasia, Moctar Ouane kuchukua nafasi hiyo. Ouane alihudumu kama Waziri wa Mambo ya Nje wa Mali kati ya mwaka 2004 na 2011.

Alikuwa mjumbe wa kudumu wa Mali katika Umoja wa Mataifa kuanzia mwaka 1995 hadi 2002 na baadaye kuwa mshauri masuala ya kidiplomasia wa muungano wa kiuchumi wa nchi za Afrika Magharibi, ECOWAS.

Uteuzi wake huenda ukachangia Mali kuondolewa vikwazo iliyowekewa na ECOWAS kufuatia mapinduzi ya kijeshi ya mwezi uliopita.

Kiongozi wa mapinduzi hayo Kanali Assimi Goita alikuwa amemteua Ndaw, ambaye aliidhinishwa rasmi Ijumaa iliyopita kuwa rais wa mpito. **BBC**



## Taarifa ulipaji kodi wa Rais Trump hadharani

**WASHINGTON D.C,** Marekani

GAZETI la New York Times, Jumapili limeripoti kwamba Rais wa Marekani, Donald Trump alilipa kodi ya dola 750 pekee mwaka aliowania urais.

Kiwango hicho alicholipa kodi ni kutoka katika mapato yake mwaka 2016, na mwaka wa kwanza alipoanza kuhudumu kama rais wa Marekani.

Gazeti hilo linasema, Rais Trump ni rais pekee katika ulimwengu wa sasa ambaye hakulipa kodi katika kipindi cha miaka 10 katika miaka 15 iliopita.

Akizungumza na waandishi wa habari Jumapili, akiwa White House, Rais Trump alitupilia mbali ripoti hiyo ya New York Times, kwa kusema ni uzishi.

Vilevile amesema kwamba licha ya huo kuwa ni uzishi, amekuwa akilipa kodi ingawaje lakini kutoa maelezo zaidi. **VOA**



## Rwanda kufungua shule licha ya corona

**KIGALI,** Rwanda

SERIKALI ya Rwanda, imesema shule zote zitafunguliwa ifikapo Novemba, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Waziri wa Elimu, Valentine Uwamariya, uamuzi wakufungua shule utaanza na vyuo vikuu.

“Shule zitafungua kwa awamu tofauti kuanzia ngazi ya vyuo vikuu ambavyo tunatarajia vitafungua milango mwezi ujao.

Shule nyingine kama sekondari, shule za msingi na chekechea tunatarajia kwamba zitakuwa zimeshafunguliwa,” alisema Uwamariya.

Wizara ya Elimu inasema, shule zitatakiwa kuzingatia masharti yaliyopo ya kujilinda na COVOD-19 kama kuwa na sehemu ya kuosha mikono, kuvaa barakoa kwa kila mwanafunzi na kuacha nafasi ya mita moja kati ya wanafunzi. **BBC**

## Saudi Arabia kuongoza mkutano viongozi G20

**RIYADH,** Saudi Arabia

SAUDI Arabia imesema, kwamba itaandaa mkutano wa viongozi wa nchi tajiri kiviwanda na zile zinazoinukia za kundi la G20.

Imeeleza kwamba mkutano huo utafanyika kwa njia ya video kutokana na janga la maradhi ya COVID-19.

Mlipuko huo wa virusi vya corona umezima matumaini ya kukusanyika katika nchi hiyo ya kifalme katika mkutano ambao ungeimarisha nafasi yake kimataifa.

Saudi Arabia ambayo ni mzalishaji mkubwa wa mafuta na mshirika mkuu wa Marekani ilichukua uongozi wa kundi la G20 katika wakati, ambapo ulimwengu umezidi kuikosoa kuhusiana na rekodi yake ya haki za binadamu baada ya mauaji ya mwandishi wa habari Jamal Khashoggi mwaka 2018 pamoja na vita vya Yemen.

Mkutano huo wa kilele wa G20 utaongozwa na mfalme Salman, mwezi Novemba mwaka huu kwa mujibu wa taarifa ya kamati ya Saudi Arabia inayohusika na G20. **VOA**

# GUARDIOLA ALIA NA MBINU ZA LEICESTER



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amelia na mbinu zilizotumiwa na Leicester, wakati timu yake ikiambulia kichapo cha mabao 5-2 nyumbani.

City walianza kutawala mchezo baada ya nyota wa zamani wa Leicester, Riyad Mahrez kuwafungia bao la kuongoza, lakini mambo yalianza kwenda kombo baada ya Jamie Vardy kusawazisha kwa penalti dakika ya 37.

"Hawakutaka kucheza, walilinda goli na kufanya mashambulizi ya kushtukiza," alisema Guardiola baada ya kushuhudia akiruhusu mabao matano kwa mara ya kwanza katika mechi 686, akiwa kocha.

"Walifunga la kwanza na penalti tatu kwa ujumla ilikuwa ngumu sana kwa upande wetu. Kukosekana kwa ubunifu kuliifanya timu yetu kutokuwa kwenye nafasi nzuri."

Huku mastraika wake wote, Sergio Aguero na Gabriel Jesus wakiwa majeruhi, City ilionekana kutokuwa na meno ya kushambulia lango la wapinzani wao.

Na mwisho wa siku walionekana kama wamechoka na Leicester ikawachapa kiurahisi huku, Vardy akifunga mara tatu 'hat-trick'.

Mabao mengine ya Leicester yalifungwa na James Maddison na Youri Tielemans.

# Ronaldo aitabiria Juventus msimu bora

**ROME,** Italia

CRISTIANO Ronaldo ametabiri "majaliwa mazuri" kwa Juventus baada ya mabao yake mawili kuisaidia kupata sare ya 2-2 dhidi ya Roma, Jumapili.

Bianconeri hao, hawakuwa na kiwango cha kuvutia pale kwenye dimba la Olimpico na walijikuta wakiwa nyuma kwa 2-1, Jordan Veretout akifunga mara mbili na Ronaldo kwa penalti.

Nafasi ya Juve kuibuka na ushindi kwenye mchezo huo iliingia doa, baada ya nyota wake, Adrien Rabiot kuonyeshwa kadi nyekundu katika dakika ya 62, lakini Ronaldo aliwahakikishia pointi moja baada ya kufunga kwa kichwa zikiwa zimesalia dakika saba, mpira kumalizika.

Licha ya Roma kutawala kwa muda mrefu, Ronaldo alifurahi kuondoka kwenye mji huo mkuu wa Italia wa Roma na pointi moja na anaamini Bianconceri wapo kwenye msimu mwingine wa mafanikio.

"Nafikiri ni suala la kupata pointi," alisema akiiambia Sky Sport Italia. "Mchezo ulikuwa mgumu na mambo yalionekana kuwa si sawa, lakini tulirudi mchezoni.

"Tuko mwanzoni tu mwa msimu, tuna kocha mpya na mawazo mapya, lakini naiona timu ikifanya vizuri.

"Nina imani tutakuwa na majaliwa mazuri zaidi kwa siku zinazokuja, hilo ni kwa uhakika kabisa.

"Tulionekana kucheza kitimu na muunganiko haukuwa mbaya, lakini naamini kabisa mambo yatakuwa mazuri tu kwa siku zinazokuja."





# *Man United kukamilisha usajili wa Sancho*

**MANCHESTER,** England

KUNA uwezekano mkubwa sasa kwa winga, Jadon Sancho kukamilisha uhamisho wake wa kwenda Manchester United.

Kocha wa Man United, Ole Gunnar Solskjaer ameiambia Borussia Dortmund kwamba, usajili wa nyota wao Sancho, utakamilika kwa wakati, kwa mujibu wa Dagbladet.

United imeripotiwa kumwania kwa muda mrefu winga huyo wa kimataifa wa England, lakini kiasi cha fedha kinachotakiwa na Borussia Dortmund kimekuwa kikwazo kwa 'Mashetani Wekundu' hao.

United haijawa tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 108 zinazotakiwa na Dortmund, ili kumwachia Sancho.

Na wakati dirisha la usajili likitarajiwa kufungwa Oktoba 5, mwaka huu, Man United sasa wameonyesha nia ya kuongeza nguvu ya kupata saini ya nyota huyo.

Aidha, Solskjaer amebainisha kwamba, wana imani kubwa ya kumsajili mchezaji huyo kwa wakati.

HABARI MICHEZO




# SIMEONE AKUNWA NA KIWANGO CHA SUAREZ

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone alivutiwa zaidi na pasi ya mwisho ya Luis Suarez na uhodari wake wa kuzunguka uwanjani, kuliko mabao yake mawili wakati Atletico Madrid wakiibuka na ushindi wa 6-1, dhidi ya Granada kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, Jumapili.

Suarez aliingizwa dakika ya 70 na kuanza kuichezea mara ya kwanza Atletico na kufunga mabao mawili na kutengeneza moja kwa Marcos Llorente.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay, ambaye alikamilisha usajili wa kujiunga na timu hiyo Ijumaa kwa euro milioni sita kutoka Barcelona, pia alishinda penalti baada ya maamuzi ya VAR.

Suarez mabao yake yote mawili aliyofunga kwa kumalizia kiufundi, moja kwa kichwa na jingine kwa kuusukumiza mpira ndani ya nyavu lakini kocha wake, Simeone alivutiwa zaidi na lile alilomtengenezea Llorente akiwa amegusa mpira kwa mara ya pili tangu aingie dimbani.

"Mabao yake mawili si kitu kwangu, lakini pasi ya mwisho ndio iliyonivutia zaidi," alisema Simeone baada ya mchezo huo.

"Mabadiliko yalitupa sisi nafasi ya ziada huku Marcos na Vitolo wakionyesha ubora wa hali ya juu pamoja na Thomas Partey na Suarez mwenyewe."

Diego Costa, Angel Correa na Joao Felix pia walifunga kwenye mchezo huo uliopigwa katika dimba la Atletico pale Wanda Metropolitano na ulikuwa ushindi mkubwa zaidi kwenye mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu kwa Simeone.

## Pirlo atetea sare Juve

**ROME,** Italia

ANDREA Pirlo amesema hajakatishwa tamaa na kiwango cha Juventus wakati wakilazimishwa sare ya 2-2 na AS Roma Jumapili, akisisitiza timu yake bado ipo kwenye "matengenezo".

Mabingwa hao wa Serie A hawakuwa katika kiwango cha kuvutia, wakati walipojikuta wakiwa nyuma kwa 2-1 kipindi cha pili, Jordan Veretout akifunga mara mbili na akafunga kwa mkwaju wa penalti.

Kiungo wa Juve, Adrien Rabiot alitolewa nje kwa kadi nyekundu muda mfupi baada ya Ronaldo kusawazisha bao kwa kichwa na kuwapa pointi moja Bianconeri hao.

Pirlo, ambaye alichukua mikoba ya Maurizio Sarri aliyefukuzwa mwezi uliopita, alibainisha kwamba kukosekana kwa ufiti wa wachezaji wake, ndiko kulikochangia matokeo hayo.

Lakini akasema anatarajia mambo yatabadilika kwa sababu timu hiyo bado inajengwa na kwamba msimu bado ni mrefu.

"Roma ilitushambulia na wachezaji wengi hivyo ulikuwa ni mchezo tofauti na Sampdoria (ambao waliwafunga 3-0 wikendi iliyopita)," alisema.

"Hii ilikuwa ni hatua nyingine, lakini timu bado inajengwa. Hatukuwa na muda wa kujaribu mbinu mbalimbali, kwani timu bado haijakaa sawa."






## Koulibaly atabakia - Napoli

**NAPLES,** Italia

MKURUGENZI wa Napoli, Cristiano Giuntoli, anaamini beki Kalidou Koulibaly atabakia kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, licha ya kuhusishwa na Manchester City na Paris Saint-Germain.

Koulibaly amekuwa akihusishwa sana na miamba ya Ligi Kuu England, City, lakini kikosi hicho cha kocha Pep Guardiola kilikubali kumsajili mlinzi wa kati wa Benfica, Ruben Dias, Jumapili.

Mabingwa wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, PSG pia wameripotiwa kumwania Koulibaly baada ya kuondoka kwa Thiago Silva.

Pia klabu za Manchester United na Liverpool, nazo awali zilikuwa zinawania kumsajili mlinzi huyo wa kimataifa wa Senegal.

Alipoulizwa kuhusu Koulibaly kabla ya mchezo wa juzi Jumapili wa ushindi wa 6-0 dhidi ya Genoa, Giuntoli aliiambia Sky Sport Italia: "Timu ilikamilika Januari kwa uwapo wa Stanislav Lobotka na Diego Demme, ambaye anaweza kucheza katika nafasi tofauti.

"Kwa uwapo wa Amir Rrahmani, (Victor) Osimhen na (Andrea) Petagna, tumekamilika, hivyo sasa tutajaribu kuwaachia wachezaji, ambao hawatakuwa na nafasi zaidi uwanjani.

"Nafikiri Koulibaly atabaki, tunafuraha kubwa, hivyo yeye ni wetu. Naamini kwamba atabakia hapa."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# AUBAMEYANG SASA AIANIKA BARCELONA

**Pia aiambia Arsenal anamtaka Aouar, akifafanua ni mchezaji mzuri na anapenda aina ya...**

**LONDON,** England

PIERRE-Emerick Aubameyang amethibisha kwamba, Barcelona ilikuwa ni miongoni mwa klabu iliyompa ofa kabla ya kusaini kuongeza mkabata na Arsenal.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, aliongeza mkataba wa miaka mitatu na 'Washikabunduki hao mapema mwezi huu, na kumaliza uvumi uliokuwa umeenea kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita.**

Barcelona imekuwa ikihusishwa na uhamisho wa nyota huyo wa kimataifa wa Gabon na Aubameyang amebainisha kwamba, walijaribu kumshawishi kwenda Camp Nou, lakini kocha wa Arsenal, Mikel Arteta alikuwa sababu tosha ya yeye kubakia na miamba hao wa London Kaskazini.

"Kulikuwa na ofa kadhaa, mojawapo kutoka Barca, lakini na klabu nyingine," alisema akiiambia Canal.

"Kipaumbele changu kilikuwa ni kubaki kwa sababu mbili: ya kwanza ni kocha, Mikel Arteta, kwa sababu tulikuwa tunazungumza mara kwa mara wakati wa 'lockdown', na alisema hapa ni nyumbani na tulizungumza mambo mengi sana.

"Bila shaka sababu ya pili, ni mapenzi niliyopata kutoka kwa watu wa klabu hii. Tangu nimefika hapa nimekuwa nikichukuliwa kama mmoja wa watoto wao, na nimeamua kubaki hapa, ni rahisi kama hivyo."

Ripoti zinadai kwamba Arsenal ilijaribu kumsajili Houssem Aouar na imetoa ofa ya euro milioni 35, ambazo zimekataliwa na Lyon, inayotaka kiasi cha euro milioni 60, ili kumuachia.

Rais wa Lyon, Jean-Michel Aulas aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter, akisema kwamba, Washikabunduki hao wanakaribia kufikia thamani ya mchezaji huyo.

Na Aubameyang amebainisha kwamba, anataka kuona timu yake hiyo ikimsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, kabla ya pazia la usajili kufungwa Oktoba 5, mwaka huu.

"Yeye ni mchezaji mzuri," alisema Aubameyang akimzungumzia Aouar. "Natumaini tutakuwa na bahati kuwa nae, kwani ni aina ya mchezaji ninayempenda."

## ZISIKUPITE

### BARCA WAMPOTEZEA MARTINEZ

BARCELONA wameachana na mipango ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 23. ***(Calciomercato)***

### UNITED YAJITOSA KWA KANTE

MANCHESTER United imewasiliana na washauri wa kiungo mkabaji wa Ufaransa, N'Golo Kante kuhusu hatua ya kuondoka Chelsea, lakini makubaliano yoyote na mchezaji huyo mwenye umri wa 29, huenda yakasababisha kupunguzwa kwa mshahara wake wa pauni 300,000 kwa wiki. ***(Mirror)***

### LAZIO KWA MATA, PEREIRA

LAZIO huenda ikataka kuwasajili viungo wawili wa Manchester United, Juan Mata mwenye umri wa miaka 32 na Mbrazili Andreas Pereira mwenye miaka 24. ***(Sun)***

### LEICESTER KUMSAJILI BREMER

LEICESTER City wanapanga kumsajili beki wa kati wa Torino mwenye umri wa miaka 23, Mbrazili Gleison Bremer, ambaye pia anawindwa na klabu ya Everton. ***(Football Insider)***

### JOSHUA AWINDWA SPURS

MSHAMBULIAJI wa Bournemouth raia wa Norway, Joshua King mwenye umri wa miaka 28, anawindwa na Tottenham Hotspur. ***(Telegraph)***

### CITY KUMWACHIA GRACIA

KLABU ya Manchester City inatarajiwa kumwachia beki kinda, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19, kurejea Barcelona, baada ya kumsajili mlinzi wa Benfica, Ruben Dias. ***(Sport)***

### PSG YAGOMA NA JORGINHO

KLABU ya Paris St-Germain imekuwa ikiwasiliana na Chelsea juu ya kumsajili kwa mkopo kiungo wa Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 28. ***(Telefoot, via Mail)***

### VILLA YAMTAKA NELSSON

KLABU ya Aston Villa imetuma maombi ya usajili ya pauni milioni tisa kwa beki wa Klabu ya Copenhagen, Victor Nelsson mwenye umri wa miaka 21. ***(Ekstra Bladet - in Danish)***

### MILAN KUMSAJILI AURIER

AC Milan wapo kwenye mazungumzo na klabu ya Tottenham kuhusu uhamisho wa beki wa kulia wa Ivory Coast, Serge Aurier mwenye umri wa miaka 27. ***(Mail)***

### BARCA WAPEWA ZINCHENKO

MANCHESTER City wamemkaribisha Barcelona kumsajili Oleksandr Zinchenko mwenye umri wa miaka 23, ambaye anamudu kucheza kama beki ama winga wa kushoto. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### SPURS YAMTAKA SEFEROVIC

TOTTENHAM pia wanapiga hesabu za kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa klabu ya Benfica na timu ya Taifa ya Uswizi, Haris Seferovic mwenye umri wa mika 28. ***(Football Insider)***

### EVERTON BADO KWA ARIAS

EVERTON bado ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili mlinzi wa Atletico Madrid na Colombia, Santiago Arias mwenye umri wa miaka 28. ***(Liverpool Echo)***

### TORINO YAJITOA KWA TORREIRA

TORINO imeondoa nia yake ya kutaka kumsajili kiungo wa Arsenal na Uruguay, Lucas Torreira, lakini Atletico Madrid ipo kwenye mbio za kumwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Mail)***

## Taifa Stars, Burundi kukipiga kwa Mkapa

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya soka ya Taifa (Taifa Stars), itacheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya majirani zao Burundi (Intamba Murugamba), itakayochezwa Oktoba 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema wageni wao wameshathibitisha kupokea mwaliko huo na mechi hiyo inachezwa siku inayotambulika kwenye Kalenda ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA).

Ndimbo alisema maandalizi ya mchezo huo yameshaanza na wachezaji watakaoingia kambini kujiandaa na mechi hiyo watajulikana Oktoba 2, mwaka huu.

Taifa Stars itatumia mechi hiyo pia kujiandaa na michezo ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika Qatar mwaka 2022 na Fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) zitakazochezwa mapema mwakani.

## Namungo yapata kikosi cha kwanza

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuvuna pointi tatu ugenini dhidi ya Mbeya City, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Theiry Hitimana, amesema sasa amepata kikosi cha kwanza, na ana matumaini mechi yao ya raundi ya sita dhidi ya Kagere Sugar timu yake itakuwa na muunganiko mzuri katika mchezo huo na inayofuata.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Hitimana alisema katika mechi tatu zilizopita ambapo walipoteza mbili ziliwaondoa katika reli wachezaji wake, lakini pia alitumia mechi hizo kutafuta kikosi cha kwanza.

Alisema baada ya mechi yao dhidi ya Mbeya City, ameanza kupata wachezaji wa kikosi cha kwanza na walicheza kwa muunganiko tofauti na mechi tatu za awali walizocheza.

"Tumeshinda mechi yetu dhidi ya Mbeya City, mchezo huo umewarudisha katika mstari wachezaji wake, tayari nimeanza kupata kikosi cha kwanza sasa nina imani ya mechi ya sita wachezaji watakuwa na muunganiko nzuri," alisema Hitimana.

Alisema sasa wamerejea nyumbani, kujiandaa na mechi yao ijayo dhidi ya Mwadui FC Jumamosi kuhakikisha wanaendelea kupata matokeo chanya katika mechi yao hiyo.

# ZAHERA AIFUNDA SIMBA KIMATAIFA

**Na Adam Fungamwango**

MKURUGENZI wa Ufundi wa Klabu ya Gwambina, Mwinyi Zahera, ameiasa Simba kutengeneza mazingira ya kuwa wazuri zaidi katika kupokonya mipira kama wanataka kufanya vema kwenye mechi za kimataifa.

Akizungumza baada ya mechi kati ya timu yake ya Gwambina dhidi ya Simba Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, timu yake ikipokea kichapo cha mabao 3-0, Zahera alisema Simba ina kikosi kizuri na wamefanya usajili mzuri msimu huu, lakini tatizo kubwa ambalo analiona litawasumbua wana udhahifu mkubwa kwenye kukaba na kukoponya mipira kwa adui.

"Simba bado hawajawa wagumu sana, japo wana kikosi kizuri, lakini kuelekea kwenye mechi za kimataifa, wanatakiwa kuwa wagumu zaidi hasa kupokonya mipira," alisema kocha huyo wa zamani wa Yanga.

**Zahera alisema Simba haiendi kucheza na timu za kawaida, bali inakwenda kucheza na timu kubwa zenye wachezaji wenye viwango vya hali ya juu, hivyo inatakiwa iwe pia na wachezaji wenye uwezo wa kukaba na si wenye kuchezesha tu timu kwenda mbele.**

"Timu kama Gwambina leo unaona tunachukua mpira na kupiga pasi mpaka 10 au 12, hii ni nzuri sana kwenye mechi kubwa za kimataifa, inachotakiwa kufanya Simba kwa kipindi hiki kifupi ni kutengeneza hali ya ugumu kwa wachezaji wake, na hasa kwenye kukaba kwa nguvu hasa kwenye viungo wake wakabaji ili kutoruhusu hali kama hiyo kwenye mechi za kimataifa," alisema.

Kuhusu kuchapwa mabao 3-0 dhidi ya Simba, Zahera alisema wala haimshangazi kwa sababu Gwambina imecheza na timu nzuri, kama ingefungwa na timu zingine zilizosalia kwenye Ligi Kuu ndiyo angeshangaa na kushtuka.

"Ujue Simba ni timu nzuri na yenye wachezaji wengi wenye uwezo, hivyo kuifunga Gwambina mabao hayo wala haishangazi, ila timu zingine zote zilizobaki kwenye ligi hakuna itakayotufunga mabao hayo," alisema Mkongomani huyo.




Meneja Masoko wa Kampuni ya M-Bet, Allen Mushi (wa kwanza kulia) katika picha ya pamoja na washindi wawili wa droo ya Perfect 12, Twalib Mfingile (wa pili kulia) na Felix Simba (wa pili kushoto), baada ya kuwakabidhi mfano wa hundi ya Sh. 79,465,240. Kushoto ni Ofisa Mwandamizi wa TRA kutoka Mkoa wa Kodi wa Ilala, Shaaban Mwanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Mashabiki wa soka washinda mamilioni ya M-BET*

**Na Mwandishi wetu**

MASHABIKI wa soka wawili nchini, kila mmoja ameshinda kiasi cha Sh. 79,465,240 baada ya kubashiri kwa usahihi matokeo ya mechi 12 za ligi mbalimbali duniani.

Mashabiki hao ni Felix Simba na Twalib Mfingile ambao wameshinda kupitia mchezo wa Perfect 12 unaondeshwa na Kampuni ya Michezo ya Kubahatisha ya M-Bet Tanzania.

Meneja masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi, aliliambia gazeti hili kuwa, washindi hao wawili wameshinda jumla ya Sh. 159,930,480 ambazo wamegawana.

Mushi alisema kampuni yao itaendelea kuwa nyuma ya mabingwa kwani washindi hao wawili ni wa tano tangu kuanza kwa msimu huu.

"Kama tulivyosema kuwa kushinda na M-Bet ni 'simple' (rahisi) tuu na Mfingile na Simba wamedhihirisha kuwa kushinda ni suala rahisi sana kutokana na aina ya mechi ambazo M-BET imekuwa ikizichagua kwa ajili ya mashabiki wa soka kubashiri," alisema Mushi.

Alisema M-BET inajivunia kuwawezesha Watanzania kwa kubadilisha maisha yao ambapo mpaka sasa jumla ya washindi watano wamepatikana kupitia michezo yao ya kubashiri," alisema Mushi.

Kwa upande wa Mfingile alisema atatumia fedha hizo kwa kilimo cha kisasa na masuala mengine ya maendeleo katika familia yake.

"Mimi ni shabiki wa mpira, lakini si kwa timu za Tanzania, napendelea zaidi timu za Ulaya na ndiyo nimeshinda kutokana na kuzifuatilia kwa ukaribu sana," alisema Mfingile ambaye ni mkazi wa Ifaraka mkoani Morogoro.

Kwa upande wa Simba alisema amejisikia faraja sana kubashiri na kushinda hasa kwa timu yake ya Arsenal ambayo inatamba sana kwenye Ligi Kuu England.

"Huwa napata ugumu sana kutabiri mechi za Manchester United, hata hivyo nilifanikiwa kubashiri matokeo yake, Arsenal ni kushinda tu," alisema Simba ambaye ni daktari mkoani Ruvuma.

Ofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa wa Ilala, Shaaban Mwanga, alisema malipo ya mashabiki hao watakatwa asilimia 18 kama kodi ya serikali.

# Michezo

Jumanne Septemba 29, 2020

Nipashe


## Aubameyang aianika Barca




# Yanga: Bao moja ni sumu, lazima ufe

**Na Mwandishi Wetu, MOROGORO**

BAADA ya timu yake kupata tena ushindi finyu wa bao 1-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Msaidizi wa Yanga, Juma Mwambusi, amesema dozi kubwa zinakuja mbeleni na kwa sasa kikubwa ni kuvuna pointi tatu, lakini akiufananisha ushindi huo sawa na sumu ambayo hata unywe nusu kijiko lazima ufe.

Tangu msimu umeanza Yanga haijawahi kushinda ama kutoka sare ya zaidi ya bao moja katika mechi nne za ligi hiyo ilizocheza hadi sasa.

Na kauli hiyo ya Mwambusi ilikuja baada ya juzi kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro na kufikisha pointi 10 zilizowapaisha hadi nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 18.

"Malengo yetu yalikuwa kupata bao dakika za mapema, lakini Mtibwa Sugar walizibana njia zetu, kikubwa ni kupata pointi tatu, Mtibwa Sugar ni timu nzito, ni timu nzuri, dhamira yetu pia ilikuwa ni kuvunja mwiko na hatimaye tumefanikiwa.

"Ushindi wa bao 1-0 si mbaya, ni sawa na sumu, ukinywa nusu kijiko, ukinywa glasi nzima, itakuua tu, huko mbele tutashinda mabao 8-0, au 10-0, tunaiandaa hiyo siku," alisema Mwambusi.

Aliongeza mechi hiyo ilikuwa ngumu hasa kipindi cha pili kwa sababu wapinzani wao walicheza kwa umoja na hatimaye kuzuia nafasi mbalimbali za kufunga ambazo walizitengeneza katika mechi hiyo.

"Tulitengeneza nafasi za kufunga tano na za wazi zilikuwa tatu, lakini hatukuzitumia vizuri, tunashukuru tumeshinda tunasonga mbele, niwasifu wachezaji wa Mtibwa Sugar kwa kucheza kiufundi, lakini kwetu ushindi umetusaidia, tumepiga hatua moja kwenda mbele," Mwambusi alisema.

Aliongeza ushindi wanaopata unasaidia kuwaimarisha wachezaji wake na wanaamini mechi zinazofuata wataibuka na ushindi mnono kama wanavyoshinda wapinzani wao, Simba.




Mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta, akiwa ameandamwa na msitu wa mabeki wa Galatasaray wakati akiichezea klabu yake ya Fenerbahce kwa mara ya kwanza kwenye mechi ya Ligi Kuu ya Uturuki iliyopigwa Uwanja wa Telekom jijini Istanbul, juzi usiku na kumalizika kwa sare tasa. Samatta ambaye aliingia dimbani katika dakika ya 66 akitokea benchi, amejiunga na Fenerbahce kwa mkopo wa mwaka mmoja akitokea Aston Villa ya England. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YATAKA YANGA ICHEZE BILA MASHABIKI

## ●●● Yapeleka barua TFF ikilalamikia namna wanavyopigwa wanapohudhuria mechi za watani zao huku...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kikosi cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kikitarajia kuondoka jijini Dar es Salaam Ijumaa kwenda Dodoma kuwakabili wenyeji wao, JKT Tanzania, uongozi wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao unajiandaa kuwasilisha malalamiko yao Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuhusiana na vurugu wanazofanyiwa mashabiki wake.

Uamuzi huo wa Simba unakuja baada ya mashabiki wa Simba kufanyiwa vurugu walipokuwa uwanjani wakati Yanga ikicheza dhidi ya Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Jamhuri mjini hapa, ikiwa ni baada ya shabiki mwingine wa Simba kupigwa na kuchaniwa jezi yake alipokuwa akiangalia mchezo wa watani zao hao wakati wa kilele cha Siku ya Mwananchi.

Baadhi ya mashabiki wa Yanga juzi katika Uwanja wa Jamhuri walionekana wakiwapiga mashabiki wa Simba kwenye mchezo huo ambao ulimalizika kwa Mtibwa Sugar kulala kwa bao1-0.

Hata hivyo, tayari Yanga imetoa taarifa kuhusu suala la mashabiki wake kufanya vurugu na kuwataka waache tabia hiyo.

Lakini Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara jana alisema Simba itawasilisha malalamiko TFF kutokana na mashabiki wake kufanyiwa vitendo visivyo vya kiungwana wanapokuwa uwanjani katika michezo mbalimbali.

Alisema anaamini shirikisho hilo litachukua hatua zinazostahiki kama lilivyofanya kwa mashabiki wa klabu nyingine ya Daraja la Kwanza ili kumaliza tatizo hilo linaloonekana kuota mizizi.

Aliwataka mashabiki na wanachama wa Simba kutolipiza kisasi na badala yake kuendelea kuwa watulivu wanapokwenda viwanjani kushuhudia michezo mbalimbali ya timu yao au klabu nyingine.

"Tunawaomba mashabiki wetu wasilipize kisasi wala kufanya vurugu kwani athari yake ni kubwa na kuna baadhi ya nchi mashabiki wao waliwahi kuzuiwa kwenda uwanjani, leo hii (jana) CEO (Ofisa Mtendaji Mkuu) wetu atapeleka barua rasmi ya klabu kwa shirikisho juu ya vitendo viovu vinavyofanywa kwa mashabiki wetu.

"Pia tunaomba baadhi ya klabu zizuiwe kuingiza mashabiki uwanjani, kwetu Wanasimba mpira ubaki kuwa burudani, Simba 'always' (mara zote) ni wastaarabu, tunaamini TFF itachukua hatua, imefika wakati sasa lazima tusema maana mashabiki wa Yanga mara zote wanakuja katika mechi zetu na hawafanyiwi vurugu, hili si jambo la kulifumbia macho," alisema Manara.

Hata hivyo, taarifa iliyotolewa jana na Ofisa Habari wa TFF, Cliford Ndimbo, ilieleza shirikisho hilo linalaani kitendo hicho kisicho cha kiungwana ambacho ni cha uvunjifu wa amani katika viwanja vya michezo.

"Vitendo hivyo havina nafasi katika mpira wa miguu na vinapaswa kukemewa na kila mpenda soka. Tunaamini vyombo vya usalama vitachukua hatua stahiki kwa waliohusika na uvunjifu huo wa amani," ilieleza taarifa hiyo jana.

Wakati huo huo, Manara alisema jana kikosi cha Simba kilichokuwa na mapumziko na kitaanza mazoezi leo kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea kuwakabili Maafande wa JKT Tanzania katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Jumapili.

Manara alisema wachezaji wote wa Simba wataanza mazoezi ya viungo leo asubuhi na jioni watahamia kwenye Uwanja wa Mo Arena ili kujiimarisha zaidi.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >